# UHUSIKA KATIKA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA KWENYE GAZETI LA *TAIFA LEO* (2017-2019)

**FIDELIS KIOKO MUTUKU**

**TASNIFU HII IMEANDIKWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**DESEMBA, 2021**

ii

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya kutahiniwa.

Sahihi________ Tarehe 16 - 12 - 2021

**FIDELIS KIOKO MUTUKU**

**C50/39142/2017**

Utafiti huu umewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sahihi________ Tarehe 16.12.2021

**DKT. JACKTONE ONYANGO**

Sahihi________ Tarehe 16.12.2021

**DKT. LEONARD CHACHA**

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa; Leonard Mutuku Mbwiko na Monicah Katiwa Mutuku, kakangu, Alphonce Mueke Mutuku na dada zangu; Emmaculate Mbula Mutuku na Magdaline Mwende Mutuku. Pia kwa marehemu dadangu, Petronila Mutinda Mutuku, Mola azidi kuilaza roho yako mahali pema penye heri. Amina!

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati nampa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uwezo wa kuvumilia mchakato mzima wa utafiti huu. Pili, nawashukuru wazazi wangu; Bw. Leonard Mutuku Mbwiko na Bi. Monicah Katiwa Mutuku kwa kunilipia karo na kuwa wavumilivu nami toka mwanzo hadi mwisho wa masomo yangu ya uzamili. Imani yenu kwangu ni ngao imara maishani mwangu, Mola awabariki na kuwazidishia. Kwa kakangu, Alphonce Mueke, dada zangu; Emmaculate Mbula na Magdaline Mwende, asanteni sana kwa utu na wosia wenu katika kipindi kizima cha masomo yangu. Kwa marehemu dadangu; Petronila Mutinda, ulikuwa nami bega kwa bega tangu mwanzo wa masomo yangu. Nakushukuru kwa mapenzi yako ya dhati na ushauri wako mwema kwangu. Mola azidi kuilaza roho yako mahali pema penye heri. Amina!

Pia, ningependa kuwapongeza wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na hasa wasimamizi wangu; Dkt. Jacktone Onyango na Dkt. Leonard Chacha kwa ushauri na maelekezo yao mema katika uandishi wa tasnifu hii. Mola awazidishie busara na utu, mzidi kuvibariki vizazi vijavyo na maarifa yayo hayo.

Shukrani zangu ziwafikie wanafunzi wenza pamoja na marafiki; Evans Kiplimo, Jemimah Ongwae, Jackline Kemunto, Osborn Wambua, Muthiani Kavoo, Kyalo Makau, Sheril, Kisambia, Thomas Mwongela, Emmanuel Mutiso, Catherine Mbithe, Kyumwa, Binnes Kalondu, Koigi, Moffat, Janet Mwikali, Yoon, Makena, Alex Maina na wengineo ambao kutangamana kwangu nao kulipevua mawazo yangu kielimu. Nawashukuru kwa motisha mliyonipa wakati wa masomo yangu.

# IKISIRI

Utafiti huu umechambua uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Matoleo ya magazeti teule ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya mwaka wa 2017 na 2019 yameongoza uchambuzi huu. Ili kufanikisha uchambuzi wa mantiki ya mada hii, nadharia ya uhusika inayoafiki malengo ya utafiti huu imetumikizwa. Malengo ya utafiti huu ni pamoja na; kudhihirisha na kuchambua dhana mbalimbali za uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*, kutofautisha majukumu na maumbo ya uhusika katika vichwa vya habari husika na kubainisha umuhimu wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu. Uhusika ni kategoria ya kisarufi ambayo huonyesha uhusiano wa viambajengo katika tungo. Aidha, uamilifu wa kila kiambajengo katika tungo na athari ya kila kiambajengo kwa viambajengo vingine huonyeshwa. Nyenzo ya data msingi ya utafiti huu ni maktaba. Mbinu ya upekuzi wa yaliyomo ilitumika katika ukusanyaji wa data hii, ambapo machapisho mbalimbali ya gazeti la *Taifa Leo* (2017-2019) yanayotawaliwa na kigezo cha siasa yalipitiwa na mtafiti kwa umakinifu kabla ya kufanywa data teule. Katika uwasilishi wa data, maelezo yameandamana na michoroti ya kisintaksia pamoja na majedwali. Kijumla, mpangilio wa kazi hii umewasilishwa kwenye sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti ulioshughulikia suala la utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Katika sura ya pili, mtafiti amebaini kuwa, miundo mbalimbali ya vichwa vya habari za siasa zina aina zifuatazo za uhusika; uhusika kiima, mahali, yambwa, tendea, tokeo na ala. Vichwa hivi vya habari huwa na kategoria mbili za uwakilisho, nazo ni; muundo ndani na muundo nje. Kwenye sura ya tatu, mtafiti ameweka wazi tofauti iliyoko kati ya majukumu na maumbo ya uhusika. Mtafiti amebainisha kuwa, majukumu ya uhusika ni dhahania ilhali maumbo yake huonekana. Umuhimu mbalimbali wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu umeelezwa ipasavyo katika sura ya nne. Baadhi ya umuhimu huo ni kurahisisha uelewaji wa sentensi katika lugha, kutambua dhima ya maneno katika tungo na kadhalika. Hatimaye sura ya tano imeangazia matokeo, changamoto na mapendekezo ya utafiti. Mtafiti ameeleza matokeo ya utafiti huu kama ifuatavyo; Kiswahili hakina maumbo dhahiri ya uhusika isipokuwa viwakilishi vya nafsi ya pili na tatu, umoja na wingi. Hata hivyo, vichwa vya habari ambavyo muundo wake hauruhusu uwepo wa viwakilishi hivi, viwakilishi ngeli vya nomino lengwa huchukua nafasi hiyo na kuwa maumbo ya uhusika. Uchunguzi huu umependekeza tafiti zaidi zifanyiwe kigezo cha uhusika kwa ajili ya kupata maarifa ziada ya kiisimu kuhusu kipengele hiki.

## ABSTRACT

This research has analysed *Taifa Leo* political topics in relation to case linguistics. *Taifa Leo* newspaper publications printed between the year 2017 and 2019 have directed this research. The case theory, which achieves the set objectives of this research has been applied to successfully complete analysis of the topic under research. The objectives of this research include; identification and analysis of several case terms found in *Taifa Leo* political topics, differentiating case roles from case grammar structures in the identified political topics and explaining the importance of case grammar in linguistics. Case is a linguistic term that shows the relationship between constituents in a phrase. Case grammar also shows the role of every constituent in a phrase and the effects of each constituent to others. The primary source of data for this research is the library. Content analysis method was used in data collection method. The researcher assembled several *Taifa Leo* newspapers published between 2017 and 2019 and purposively sampled the ones with political topics for study. Data was presented in a descriptive manner whereby, syntactical drawings and tables accompanied with illustrations were used. In general, this research is made up of five chapters. Chapter one consists of research introduction which is made up of; statement of the problem, objectives of the study, scope and limitation of the study, theoretical framework and research methodology. In chapter two, the researcher has identified that different structures of political topics have got the following types of cases; nominative case, locative, accusative, dative, factitive and instrumental. These topics have got two categories of representation, which include; deep structure and surface structure. In chapter three, the researcher has clearly shown the difference between case roles and structure. The researcher has identified that case roles are covert while structures are overt. In chapter four, the researcher has explained several importances of case grammar in Kiswahili linguistics. Such importances include; easing sentence understanding in language, identifying the role of words in a clause, etc. In chapter five, findings of this research, challenges and recommendations have been well presented. The findings of this research have clearly shown out that, Kiswahili does not exhibit any overt case structures except in second and third person pronouns, singular and plural. However, if the political topic structure doesn't accommodate second and third person's pronoun, therefore, a correct pronoun that matches the class of the targeted noun in that structure is used as a case form. This study has recommended more research to be done on the field of grammatical cases for the purpose of generating more linguistic knowledge about them.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

| | |
|---|---|
| Siasa | Ni mfumo wa kiitikadi unaotumiwa na kikundi cha watu au jamii fulani kuendeshea serikali pamoja na shughuli za jamii hiyo. |
| Uhusika | Hii ni dhana ya kisarufi itumiwayo kuonyesha dhima ya maneno katika tungo. |

## VIFUPISHO NA ISHARA

| | |
|---|---|
| AL | Uhusika Ala |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| HL | Hali |
| K | Ishara za uhusika |
| KIM | Kiima |
| KL | Kauli |
| KN | Kirai nomino |
| N | Nomino |
| NMG | Nation Media Group |
| MH | Uhusika mahali |
| Ø | Mofu kapa |
| PM | Uhusika pamoja |
| S | Sentensi |
| T | Kitenzi |
| TD | Uhusika tendea |
| TK | Uhusika tokeo |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UH | Uhusika |
| YA | Uhusika yambwa |
| W | Kiwakilishi |
| W.nf.2w | Kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi |
| W.nf.3u | Kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja |

# YALIYOMO

IKISIRI ........ v
ABSTRACT ........ vi
UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU ........ vii
VIFUPISHO NA ISHARA ........ viii
SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI ........ 1
1.0 Usuli wa Mada ........ 1
1.1 Suala la Utafiti ........ 3
1.2 Malengo ya Utafiti ........ 5
1.3 Maswali ya Utafiti ........ 5
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........ 5
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 7
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ........ 7
1.7 Misingi ya Nadharia ........ 12
1.7.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhusika ........ 18
1.7.2 Aina za Uhusika ........ 18
1.8 Mbinu za Utafiti ........ 20
1.8.1 Eneo la Utafiti ........ 20
1.8.2 Muundo wa Utafiti ........ 20
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli ........ 21
1.8.4 Mbinu za Ukusanyaji Data ........ 22
1.8.5 Maadili ya Utafiti ........ 22

1.8.6 Uchanganuzi wa Data....23

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo....23

1.9 Hitimisho....24

SURA YA PILI....25

UHUSIKA KATIKA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA....25

2.1 Utangulizi....25

2.1.1 Uhusika Kiima....26

2.1.2 Uhusika Mahali....30

2.1.3 Uhusika Yambwa....34

2.1.4 Uhusika Tendea....38

2.1.5 Uhusika Tokeo....42

2.1.6 Uhusika Ala....47

2.2 Hitimisho....51

SURA YA TATU....52

TOFAUTI KATI YA MAJUKUMU NA MAUMBO YA UHUSIKA KATIKA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA....52

3.0 Utangulizi....52

3.1 Tofauti kati ya Majukumu na Maumbo ya Uhusika....52

3.1.1 Tofauti kati ya Jukumu Mtendi na Umbo la Uhusika Kiima....56

3.1.2 Tofauti kati ya Jukumu Mahali na Umbo la Uhusika Mahali....59

3.1.3 Tofauti kati ya Jukumu Ala na Umbo la Uhusika Ala....63

3.1.4 Tofauti kati ya Jukumu Mtendwa na Umbo la Uhusika Yambwa....65

3.1.5 Tofauti kati ya Jukumu Tendea na Umbo la Uhusika Tendea....68

3.1.6 Tofauti kati ya Jukumu Tokeo na Umbo la Uhusika Tokeo ....................70

3.2 Hitimisho....................73

SURA YA NNE....................74

UMUHIMU WA SARUFI UHUSIKA KATIKA TAALUMA YA ISIMU....................74

4.0 Utangulizi....................74

4.1 Umuhimu wa Sarufi Uhusika katika Taaluma ya Isimu....................74

4.1.1 Kurahisisha Uelewaji wa Sentensi katika Lugha....................74

4.1.2 Kutambua Dhima ya Maneno katika Tungo....................75

4.1.3 Usarufi wa Tungo....................76

4.1.4 Kukua kwa Matumizi ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili ambazo Msingi wake ni Sarufi Zalishi....................78

4.2 Hitimisho....................82

SURA YA TANO....................84

HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO....................84

5.1 Utangulizi....................84

5.1.1 Muhtasari wa Utafiti....................84

5.1.2 Matokeo ya Utafiti....................86

5.1.3 Changamoto ya Utafiti....................89

5.1.4 Mapendekezo....................89

5.2 Hitimisho....................90

Marejeleo....................91

KIAMBATISHO A....................98

PICHA ZA MAGAZETI YA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA TEULE VYENYE UHUSIKA LENGWA....................98

1. Uhusika Kiima....................98

2. Uhusika Mahali ........................................................................ 99
3. Uhusika Yambwa ...................................................................... 101
4. Uhusika Tendea ....................................................................... 102
5. Uhusika Tokeo ......................................................................... 104
6. Uhusika Ala ............................................................................. 105
KIAMBATISHO B ............................................................................ 107
KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA CHUONI ..................................... 107
KIAMBATISHO C ............................................................................ 108
KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA NACOSTI ................................... 108

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Uhusika ni dhana ya kisarufi ambayo hutumiwa kuonyesha dhima ya maneno katika tungo. Dhana hii ni muhimu katika uchambuzi wa tungo kwani hunuia kuwasilisha ujumbe wa kisemantiki uliogubikwa katika muundo wa ndani. Wanauhusika husema kuwa, semantiki ndio msingi mkuu wa lugha bali si sintaksia. Katika semantiki, lugha hueleweka, hupitia mifanyiko mbalimbali, huhifadhiwa na kutumika. Chafe (1970) anasema kuwa, uhusika hunuia kutambua ruwaza za kijumla za muundo wa ndani wa mwingiliano wa lugha. Ruwaza hizi zimeelezwa kama muundo wa ndani wa kisemantiki ambao huashiria mahusiano ya maana ya maneno katika sentensi. Wanauhusika husema kuwa, semantiki ndio msingi mkuu wa lugha bali si sintaksia. Katika semantiki, lugha hueleweka, hupitia mifanyiko mbalimbali, huhifadhiwa na kutumika.

Kwa mujibu wa Fillmore (1968), kimuundo, lugha huwa na kategoria mbili ambazo ni; muundo wa ndani na muundo wa nje. Muundo wa ndani huwa ni wa kidhahania kwani huwakilisha yale maoni ambayo mtunzi wa sentensi hutarajia kuyatumia katika utunzi wake. Huu ni muundo ambao huhusisha msamiati hitajika wa sentensi na hubainisha mahusiano ya kisarufi kwa kila mojawapo. Muundo wa ndani huwakilisha vigezo vya kimsingi vya maana katika sentensi. Muundo wa nje ni lile umbo la sentensi ambalo huonekana. Ndipo uhusika utende kazi, miundo ya

ndani na ya nje katika sentensi yafaa kufahamika na kutofautishwa kwa uwazi. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa uhusika ni dhana ambayo huchambua na kuchanganua lugha kwa kuzingatia muundo wake wa ndani na wa nje. Vivyo hivyo, ndivyo vichwa vya habari vya kisiasa katika gazeti la *Taifa Leo* vilivyochanganuliwa.

Kwa mujibu wa BAKITA (2015), gazeti ni chapisho linaloundwa kwa karatasi nyembamba na pana na ambalo huwa na nia maalumu ya kupasha watu habari. Habari hizi huwa za mambo yanayojiri katika jamii. Baadhi ya mambo hayo ni siasa, uchumi, usalama, elimu, dini, utalii, maendeleo ya kijamii na kadhalika. Kando na redio, runinga, tovuti, majarida na mitandao mingine ya kielektroniki, gazeti ni mojawapo ya vyombo maalumu na maarufu vya kusambaza habari zinazojiri katika jamii. Aghalabu, habari hizi huwa za kuaminika kwani kamati ya uchapishaji huzipiga msasa kabla ya kuzichapisha kwa ajili ya kutowapotosha wanajamii. Kutokana na suala la uchapishaji, habari hizi hudumu jinsi zilivyo pasipo na mabadiliko ya mara kwa mara kinyume na habari za redio na runinga ambazo uwasilisho wake hubadilikabadilika kulingana na zamu ya mtangazaji habari. Mabadiliko haya huweza kukuza maana mbadala kinyume na maana asilia kutokana na jinsi taarifa hiyo ilivyowasilishwa. Maana katika vichwa vya habari vya kisiasa katika gazeti hubakia jinsi zilivyonakiliwa. Kuna magazeti mbalimbali nchini Kenya, nayo ni pamoja na; gazeti la *Taifa Leo*, *People's Daily*, *The Standard*, *Daily Nation, The Star, Mwanaspoti, Sunday Nation, Saturday Nation, Pambazuka* na kadhalika. Waandishi, wachapishaji pamoja na wahariri wa

magazeti haya huwa na malengo maalum ya kuwajuza wanajamii kuhusu mambo yanayoendelea nchini. Masuala ya kisiasa ni mojawapo ya habari ambazo zimetamalaki katika magazeti haya.

BAKITA (2015) wameeleza siasa kama mfumo wa kiitikadi unaotumiwa na kikundi cha watu au jamii fulani kuendeshea serikali pamoja na shughuli za jamii hiyo. Shughuli hizi hulenga kuboresha hadhi ya mtu au kuongeza uwezo wa kimadaraka ndani ya asasi fulani. Utafiti uliotekelezwa, umeangazia vichwa vya habari vya siasa vilivyonuia kuendesha shughuli za serikali. Vichwa hivyo vya kisiasa vimeteuliwa kimakusudi kutoka kwa magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya mwaka 2017 – 2019, kwa sababu ni kipindi cha hivi karibuni nchini Kenya kutamalakiwa na masuala ya siasa. Ni wazi kuwa, baadhi ya vichwa hivyo vimekusudia kuboresha hadhi ya kiongozi fulani kisiasa huku vingine vikiashiria kumkuza na kumjenga kimadaraka. Hata hivyo, kuna vichwa vya habari za siasa ambavyo vilisuta na kuukaripia utawala wa viongozi fulani katika jamii. Utafiti huu umejikita katika kuchanganua vichwa vya habari vya kisiasa vilivyoko katika gazeti la *Taifa Leo* pekee. Dhana ya uhusika hutawala muundo wa vichwa vya habari vya siasa katika gazeti la *Taifa Leo*.

## 1.1 Suala la Utafiti

Utafiti huu umejikita katika uchunguzi wa jinsi uhusika ulivyojitokeza katika vichwa vya habari za siasa vilivyoko kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Kujitokeza kwa kipengele hiki cha sarufi cha uhusika kumefumbua fasili yenye usawa wa kimaana katika vichwa teule vya habari za siasa, kinyume na fasili nyingine binafsi ambazo

hutegemea upana wa mawanda ya fikra za wasomi na uelewaji wao wenyewe. Fasili hizi za kibinafsi hutofautiana kutoka kwa msomi mmoja hadi mwingine. Hivyo basi, maana mbalimbali za kichwa kimoja cha habari ya siasa huweza kuibuliwa na kusababisha utata wa kimaana katika ujumbe husika. Kigezo cha uhusika ambacho hujikita kwenye dhima ya neno katika tungo kimeweza kusuluhisha utofauti huu wa maana. Kigezo hiki kimetumika kama kielelezo cha kufasili maana kwenye tungo lengwa. Kwa kufanya hivyo, wasomaji wa gazeti wameweza kudondoa maana sawia ibebwayo na vichwa hivyo vya habari kwa urahisi, ukamilifu na uwazi. Pia, udondozi huo wa maana umewapa wasomaji wa magazeti mwanga wa masuala yanayokusudiwa kuangaziwa katika makala yote ya kisiasa, hivyo basi, kuwarahisishia uelewaji wakati wa usomaji.

Kwa ufahamu wangu, kutokana na utafiti wa awali niliotekeleza, hakuna utafiti wa kiisimu unaohusisha kipengele cha uhusika katika uchambuzi wa makala ya gazeti lolote lile uliofanywa. Tafiti nyingi za hivi majuzi zimechambua vipengele vya fasihi kama vile maudhui ya ushairi na usawiri wa wahusika katika makala ya gazeti. Tafiti ambazo ni za kiisimu zimejikita katika kutoa maoni, kukosoa na kutathmini makala ya tafsiri yaliyoko gazetini. Pia, wanasarufi wachache wamedokezea dhana ya uhusika bali hawakuichunguza kama mada kuu hasa katika Kiswahili, hivyo basi, hilo ni pengo ambalo lilifaa kufidiwa.

### 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umenuia kuafikia malengo yafuatayo:

1. Kudhihirisha na kuchambua dhana mbalimbali za uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*.
2. Kutofautisha majukumu ya uhusika na maumbo ya uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*.
3. Kubainisha umuhimu wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umedhamiria kujibu maswali yafuatayo:

1. Uhusika hujitokeza vipi katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*?
2. Ni vipi majukumu na maumbo ya uhusika hutofautiana katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*?
3. Sarufi uhusika ina umuhimu gani katika taaluma ya isimu?

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii imechaguliwa kwa sababu ya uwepo wa data ya kutosha kutoka kwa magazeti anuwai ya *Taifa Leo*, tasnifu zilizoandikwa awali baada ya kutafiti masuala yanayohusiana na makala ya magazetini, matumizi ya mtandao na vitabu mbalimbali vya urejelezi. Pia, huu ni utafiti ulio na umuhimu wa kisarufi, kinadharia na kiutendakazi katika Kiswahili. Kwa upande wa sarufi ya Kiswahili, uchaguzi wa mada hii umetokana na mchango wake katika usomi wa isimu ya Kiswahili. Kisintaksia, utafiti huu ni muhimu kwa sababu umeshughulikia dhima

ya maneno katika sentensi. Kwa mujibu wa Bussman (1996), kuna aina tatu za dhima; dhima zinazotegemea leksimu, dhima zinazotegemea majukumu ya kisarufi ya kileksimu na zile zinazotegemea majukumu ya kisemantiki. Hata hivyo, baadhi ya dhima ambazo huhusishwa na maneno ni pamoja na; uhusika kiima, uhusika yambwa, uhusika tendea na uhusika tokeo. Dhima hizi za maneno katika tungo zimewaongoza wasomi wa magazeti kudondoa maana bia katika vichwa husika vya habari za kisiasa, hivyo kuondoa utata wa kimaana. Kinadharia, uchujaji wa dhima umetekelezwa ili kuhakikisha uzingativu wa kanuni za uhusika. Uhusika hunuia kuwasilisha ujumbe wa kisemantiki ambao hugubikwa katika muundo wa ndani. Kiutenda kazi, mfumo wa modeli ya uhusika, wake Fillmore (1968), na kanuni tatu kuu za utiaji uhusika zimehusisha sentensi vilivyo kwa kuangazia mahusiano ya kiuhusika yaliyopo katika sentensi. Pia, maumbo na majukumu ya uhusika katika isimu yamebainishwa.

Mada nzuri ya utafiti ni ile ambayo haijatafitiwa mno na wasomi na ambayo huibua maarifa mapya katika taaluma ya usomi. Kimalu na Marimba (2014) wanasema kuwa utafiti una jukumu la kuibua maarifa mapya, hoja mpya na mitazamo mipya pamoja na utenda kazi wake. Vivyo hivyo, mada ya utafiti huu imechaguliwa kwa sababu hizo. Maarifa mapya ya jinsi uhusika hutumika katika uandishi wa habari zilizojiri katika magazeti yameibuliwa. Vile vile, umuhimu wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu umebainishwa. Kwa kufanya hivi, taaluma ya isimu imepanuliwa kiusomi kwa kuwepo tafiti mbalimbali za isimu zinazoshughulikia makala ya magazeti kinyume na ilivyo kwa sasa.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Katika utafiti unaotekelezwa, gazeti la *Taifa Leo* ndilo upeo na mipaka ya utafiti. Magazeti mengine kama vile; *The Star*, *People's Daily*, *The Standard Nation* na kadhalika, yangeangaziwa lakini gazeti la *Taifa Leo* limepewa kipaumbele kwa kuwa kampuni ya Nation Media Group (NMG) hulichapisha kila siku. Hivyo basi, hili ni gazeti linalopatikana kwa urahisi katika sehemu nyingi nchini Kenya. Gazeti la *Taifa Leo* limeandikwa kwa Kiswahili kinyume na magazeti mengine, hivyo basi, limefaa katika utafiti huu. Baadhi ya magazeti ya Kiswahili kama vile *Pambazuka* na *Mwanaspoti* hayangeweza kutegemewa kwani huchapishwa baada ya kipindi fulani na kipindi cha uchapishaji huo chaweza kukosa masuala ya kisiasa, hivyo basi, kutojumuishwa katika habari zilizojiri.

Marshall na Rossman (1995) wanasema kuwa, upeo katika utafiti waweza kuwa mpana au finyu kulingana na suala la utafiti na malengo ya kazi ya utafiti. Ni wazi kuwa gazeti la *Taifa Leo* huwa na habari mbalimbali zilizojiri katika jamii kama vile masuala ya michezo, lugha, afya, ugatuzi na maendeleo ya nchi, masuala ya nchi za kigeni na kadhalika. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika uchambuzi wa vichwa vya habari za siasa pekee.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Utafiti wa maktabani umedhihirisha kuwa tafiti nyingi ambazo zimeshughulikia makala ya magazetini zimejikita katika vipengele vya fasihi kinyume na utafiti wa kiisimu unaotekelezwa. Karichia (2012) alilenga kubainisha na kutathmini jinsi

waandishi wa habari katika magazeti, hasa gazeti la *Taifa Leo* husawiri wanasiasa kama wahusika katika miktadha maalumu ya kisiasa. Huu ni utafiti ambao umebainisha wazi jinsi sifa za wanasiasa hubadilikabadilika kulingana na tukio. Wanasiasa huwa ni wenye huruma katika muktadha wa msiba na wachangamfu katika muktadha wa kuadhimisha sikukuu za kitaifa. Utafiti huo ulitilia mkazo matumizi ya lugha, watumizi wake na majukumu ya lugha katika jamii. Ni kweli kuwa utafiti huo ulichambua makala ya kisiasa katika gazeti la *Taifa Leo* sawia na utafiti unaotekelezwa. Hata hivyo, kuna tofauti kati ya utafiti wa Kachiria (2012) na utafiti unaotekelezwa. Tofauti hiyo ni kuwa, utafiti unaotekelezwa umeangazia dhima ya maneno katika vichwa vya habari vya kisiasa kinyume na utafiti wa Kachiria (2012).

Utafiti wa Magoma (2015) umeshughulikia fani na maudhui katika mashairi ya magazeti ya *Taifa Leo Jumamosi* na *Taifa Jumapili* katika kipindi cha mwaka 2010-2012. Magoma (2015) alitumia nadharia kimtindo ya urasimi iliyoasisiwa na Leech na Short (1981). Nadharia hii iliteuliwa kwa msingi kuwa mihimili yake ingefanikisha kusawiri maudhui teule katika mashairi ya magazeti ya *Taifa Leo* ili kuafikia malengo ya utafiti wake. Maudhui teule yaliyoangaziwa ni pamoja na, maudhui ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Huu ni utafiti uliobainisha nafasi ya magazeti ya *Taifa Leo* katika maendeleo ya mashairi nchini Kenya. Ni kweli kuwa utafiti wa Magoma (2015) una mshabaha kiasi na utafiti unaotekelezwa kwani tafiti zote zimejikita katika aina moja ya gazeti ambalo ni gazeti la *Taifa Leo*. Hata hivyo, tafiti zote zina tofauti kubwa mno kwani Magoma (2015) alijikita katika

fasihi kwa kusawiri maudhui ya siasa ilhali utafiti unaotekelezwa unaangazia kipengele cha lugha cha uhusika katika mada za habari za kisiasa katika gazeti hilo. Kinyume na kubainisha nafasi ya magazeti ya *Taifa Leo* katika maendeleo ya mashairi nchini Kenya, utafiti unaotekelezwa unabainisha umuhimu wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu.

King'ori (2005) ametekeleza utafiti wa kiisimu ambao umeangazia suala la uhamaji wa maneno katika sentensi ya Kiswahili. Utafiti wake umejikita katika tawi la isimu la sintaksia jinsi ilivyo katika utafiti unaotekelezwa. Katika utafiti huo, King'ori (2005) ameeleza na kuonyesha sifa bainifu za kimuundo za kauli ya kutoa taarifa na jinsi nomino na vitenzi huhama katika sentensi ya Kiswahili. Pia, ameangazia aina za maumbo ya uhamaji ambazo hupatikana katika sentensi ya Kiswahili. Utafiti huu wa uhamaji huhusisha maelezo ya viambajengo vya sentensi, kanuni na masharti mahususi ambayo hushurutisha muundo wa sentensi ya Kiswahili. Kanuni ya uhusika chujaji imetumika katika utafiti wa Kingori (2005) ndipo kuhakikisha kuwa kila kiima wazi kimepewa uhusika dhahania. Matumizi yake huhakikisha uchujaji wa muundo wowote ulio na kiima wazi ambacho hakijapewa uhusika. Sentensi huwa si sahihi kisarufi kama haijapewa uhusika wowote. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa King'ori (2005) na unaotekelezwa ni kuwa, utafiti wa King'ori umejikita katika kipengele cha sarufi cha uhamaji katika sentensi ya Kiswahili ilhali utafiti unaotekelezwa umejikita katika kipengele cha sarufi cha uhusika katika mada za habari za kisiasa katika gazeti la *Taifa Leo*.

Nyongesa (2005) ametekeleza utafiti wa diskosi katika tahariri za magazeti yafuatayo; *Kenya Times, People's Daily, East African Standard* na *Sunday Nation*. Huu ni utafiti ulioongozwa na nadharia ya muundo balagha iliyoasisiwa na Mann na Thompson (1987) na modeli ya Hatch (1992). Utafiti wake umejikita katika uchunguzi wa miundo balagha ya tahariri za magazeti teule. Huu ni utafiti uliobaini iwapo tahariri katika diskosi ya magazeti nchini Kenya huridhisha wasomi wa habari kupitia kwa mantiki razini yanayovutia au kupitia kwa mvuto wa mhemuko usiokuwa razini. Pia, utafiti huu umebainisha kuwa, tahariri katika magazeti ya Kiingereza zina sifa shawishi ya diskosi kuliko diskosi hoja. Tahariri zina mvuto wa mhemuko wa maadili kuliko mvuto wa mantiki razini yanayotarajiwa. Kulingana na muundo wake, tahariri za magazeti ya Kiingereza hutilia maanani muundo wa kiwango cha juu wa hoja. Hii ni kumaanisha kuwa tahariri huwa na muundo wa mukhtasari wa matukio, ushahidi na koda ya kipragmatiki. Muundo wa viambajengo vya tahariri kama hoja ya diskozi hubainishwa kwa mahusiano halisi ya kishazi hata ingawa baadhi kama vile; tathmini na mahusiano kinyume hupatikana katika miundo yote mitatu ya viambajengo. Utafiti wa Nyongesa (2005) ulichanganua tahariri katika magazeti manne teule ya Kiingereza ilhali utafiti unaotekelezwa umechanganua uhusika katika vichwa vya habari vya siasa katika gazeti la *Taifa Leo* pekee ambalo limeandikwa kwa Kiswahili.

Utafiti wa Naswa (2003) umeegemea tawi la isimu la sintaksia jinsi ilivyo katika utafiti unaotekelezwa. Utafiti wake ulichanganua uhamaji wa kirai nomino katika

sentensi ya Kiswahili. Alibainisha kuwa, kirai nomino kina uwezo wa kuhama kutoka kwa nafasi ya kiima ya kishazi cha chini hadi kwa nafasi ya kiima ya kishazi cha juu katika sentensi changamano. Kwa mujibu wa Cook (1988), kirai nomino chaweza kuhama na kuchukua nafasi kapa lakini si nafasi ambayo tayari keshajazwa. Utafiti wa Naswa (2003) umeongozwa na nadharia ya utawala na ufungami ambayo ndani yake kuna kijinadharia cha uhusika ambacho kimetumika kuweka uhusika dhahania kwa virai nomino vyote. Uhusika huo hutolewa kulingana na uamilifu wa kisarufi wa mahali ambapo kirai nomino hicho hupatikana. Kanuni ya uhusika chujaji ya nadharia ya uhusika imetumika katika utafiti wake ndipo kuelezea ni kwa nini uhusika hutokea katika kauli tendwa na sentensi dakizi. Hata ingawa kuna mshabihiano wa matumizi ya nadharia ya uhusika iliyo na kanuni chujaji ya uhusika, kinyume na utafiti huu, utafiti unaotekelezwa unaongozwa na nadharia ya uhusika pekee bali si vijinadharia vyote vya utawala na ufungami. Utafiti huo unachanganua vichwa vya habari za siasa katika gazeti la *Taifa Leo* bali si sentensi ya Kiswahili.

Utafiti wa Kaviti (2005) ni wa kiisimu. Mtafiti huyu alishughulikia makosa ya kisintaksia katika tafsiri za makala gazetini. Alirejelea gazeti la *Taifa Leo* kama ilivyo katika utafiti unaotekelezwa. Hata hivyo, tofauti kuu kati ya utafiti wake na unaotekelezwa ni kuwa, utafiti wake ulijikita katika kutathmini na kukosoa kazi za tafsiri katika makala ya gazeti ilhali utafiti unaotekelezwa umejikita kuangazia dhana ya uhusika katika vichwa vya habari za siasa vilivyo katika gazeti la *Taifa Leo* bali si makala yaliyomo gazetini.

Ni wazi kuwa, tafiti za awali zilizotekelezwa ni tofauti sana na utafiti unaofanywa. Baadhi ya tafiti hizo ni pamoja na tafiti za Karichia (2012) na Magoma (2015) ambazo zimeegemea kipengele cha fasihi ilhali utafiti unaofanywa ni wa kiisimu. Hata hivyo, tafiti za kiisimu ambazo zimefanywa zimeangazia mno kipengele cha uhamaji wa maneno katika sentensi ya Kiswahili kinyume na utafiti unaotekelezwa, ambao umeangazia dhima ya maneno katika tungo. Tafiti hizi zimetekelezwa na Naswa (2003) na King'ori (2005). Magazeti teule aliyotumia Nyongesa (2005) katika utafiti wake ni tofauti na gazeti teule linalotumika katika utafiti huu. Hata ingawa Kaviti (2005) alitumia gazeti la *Taifa Leo* katika utafiti wake, inabainika kuwa yeye alijikita katika makala yote bali si vichwa vya habari pekee.

**1.7 Misingi ya Nadharia**

Charles J. Fillmore ni mwanaisimu wa Kimarekani aliyezaliwa mnamo mwaka wa 1929 na ndiye mwasisi wa nadharia ya uhusika (Fillmore, 1968). Kwa mujibu wa Chafe (1970), Fillmore alikuwa mmoja kati ya wanaisimu ambao waliasisi uwakilisho wa utambuzi wa kiisimu ambao ulibainisha tofauti kati ya utambuzi wa lugha kisintaksia na kisemantiki. Muundo wake wa uhusika wa kisarufi uliwavutia mno wanasaikolojia na wanaisimu kokotozi. Kabla ya kuiasisi nadharia ya uhusika, Fillmore alikuwa mwitifaki wa nadharia ya sarufi zalishi yake Noam Chomsky. Katika tafiti zote alizotekeleza Fillmore, ameonyesha umuhimu mkuu wa semantiki na dhima yake katika kuyapa motisha masuala yanayohusiana na sintaksia na mofolojia. Mtazamo wa Fillmore (1968) kuhusu nadharia ya uhusika umejikita katika misingi miwili mikuu. Misingi hii ni;

a) Kitovu cha sintaksia

b) Kategoria fiche

Msingi wa kitovu cha sintaksia ni mtazamo ambao hutenda kazi kutoka umbo la mofolojia na maumbo mengine ya matawi ya isimu yaliyo chini ya umbo hili. Msingi huu hujikita katika matumizi maana ya kategoria za uhusika za kimapokeo. Kanuni za umbo la kisemantiki ni miundo ya ndani iliyoundwa na modeli ya uhusika ya 1968 ambayo hubainishwa kwa sifa zifuatazo;

1. Sentensi hutenganishwa kwa kauli na hali.

S (Sentensi) ⟶ KL (Kauli) + HL (Hali)

Kauli ni seti za mahusiano yanayohusisha vitenzi na nomino zisizokuwa na njeo ilhali hali huhusisha ukanushi, njeo na kadhalika.

2. Kauli huhusisha kitenzi na mfuatano wa uhusika kutoka kulia hadi kushoto.

KL (Kauli) ⟶ T (Kitenzi) + UH (Uhusika) + $UH_n$... (Mfuatano wa uhusika)

Kauli huhusisha kitenzi na mfuatano wa ishara za uhusika za kirai nomino. Kitenzi huwekwa upande wa kushoto huku dhana za uhusika zilizo na mahusiano zikiorodheshwa kwa mpangilio kutoka sehemu ya kulia hadi kushoto pamoja na chaguo la kiima kilicho na uwezekano kwenye sehemu ya kulia katika muundo wa ndani. Fillmore anaongeza kuwa angalau kategoria moja ya uhusika yafaa kuchaguliwa na hakuna kategoria ya uhusika inayofaa kutokezea mara zaidi ya moja.

3. Ishara za uhusika hutokea katika muundo wa ndani.

UH (Uhusika) ⟶ K (Ishara ya uhusika) + KN (Kirai nomino)

Kila uhusika huhusisha ishara za uhusika na kirai nomino, ambapo ishara za uhusika hutanguliza kirai nomino katika muundo wa ndani. Ishara za uhusika ni kipengele bia cha lugha ambacho chafaa kutambulika kama kihusishi na kiambishi uhusika.


Katika uwasilishaji wa muundo msingi wa sentensi, kanuni hizi tatu hutumika kwa utaratibu rasmi. Dhana moja au mbalimbali za uhusika kama vile ala, mhusika, mtendi, yambwa na kadhalika hupishwa nafasi katika kategoria za uhusika za kanuni ya pili. Ishara za uhusika halisi ambazo huhusiana na uhusika hutiwa katika kanuni ya tatu. Mchoroti ufuatao unaonyesha jinsi uhusika hutiwa katika sentensi.

**Mchoroti 1.1: Utiaji uhusika**

John alivunja dirisha kwa nyundo

John/ alivunja/ dirisha/ kwa nyundo

KIM T YA AL





Kanuni ya kwanza kwenye mchoroti 1.1 limegawa sentensi, *John alivunja dirisha kwa nyundo* katika sehemu mbili kuu; sehemu ya kwanza ni hali. Hii ni sehemu ambayo huonyesha wakati kitendo kilitendeka. Katika kielelezo hiki, kitendo vunja kilitendeka wakati uliopita. Sehemu ya pili ni kauli. Sehemu hii inahusisha seti za mahusiano kati ya kitenzi na nomino. Seti hizo za mahusiano ni kati ya kitenzi, *vunja* na nomino, *John*, *dirisha* na *nyundo*. Mahusiano haya ndiyo yanayojitokeza katika kanuni ya pili. Hivyo basi, kitenzi, *vunja* kinafuatwa na aina mbalimbali za uhusika; uhusika yambwa, uhusika ala na uhusika kiima kama ilivyo katika kielelezo. Kabla ya kutia uhusika kwenye virai nomino, *John*, *dirisha*

na *nyundo* ishara ya uhusika, *K* imetanguliza virai nomino hivi. Pale ambapo kirai nomino hutangulizwa na kihusishi, kihusishi hicho huwa ishara ya uhusika. Pale ambapo kirai nomino hakitangulizwi na kihusishi, ishara kapa, *Ø* huchukua nafasi ya ishara uhusika. Katika uhusika yambwa, kirai nomino dirisha kimetangulizwa na ishara kapa ya uhusika huku vihusishi, *kwa* na *na* vikitanguliza virai nomino, *nyundo* na *John* ambavyo vimebeba uhusika ala na kiima mtawalia.

Fillmore (1987) anasema kuwa, aina mbalimbali za makundi ya vitenzi na uwekaji wa virai katika makundi mbalimbali yaweza kubainishwa kimaana zaidi iwapo, miundo ambayo vitenzi hivyo vilihusishwa nayo mwanzoni ingeelezwa kwa kigezo cha dhima kisemantiki ya hoja zinazohusiana. Alipendekeza kuwa, kimsingi vitenzi vinapaswa kuchukuliwa kuwa na sifa ya muundo wa ndani ambao ni maelezo ya valensi yaliyofafanuliwa kwa kigezo cha uhusika kiunzi pamoja na maelezo yaliyoegemezwa kwa kanuni. Uhusika huwa wa aina mbalimbali. Kila fahiwa kitenzi hukubali sehemu ya kikundi cha aina hizi za uhusika. Vijikundi hivi hugawika katika seti za lazima na zisizo za lazima. Mfano wa elementi za uhusika ni; ajenti, mhusika, tokeo, mtendwa, njeo, lengo na kadhalika. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha jinsi muundo wa uhusika ulivyo.

**Kielelezo 1.1: Muundo wa uhusika**

Joel alimpa Joy kitabu.




-Tukio lilikuwa gani?

- Ni nani alitenda kitendo?

- Ni nani alitendewa kitendo?

- Ni nini kilihusishwa kwa kitendo?

- Kitendo kilitendwa lini?

Joy alipewa kitabu na Joel.

Kielelezo hiki hubainisha kuwa katika fahiwa ya kitenzi kuna seti ya uhusika. Baadhi ya seti hizo huwa za lazima huku nyinginezo zikiwa si za lazima. Uhusika ni lazima uwepo katika sentensi na uondolewapo, sentensi husika hubakia kutokuwa sahihi kisarufi. Kutokana na mchoro huu wa uwakilisho wa muundo wa uhusika kunabainika sifa mbili zifuatazo;

a) Aina za uhusika zinazohusishwa na kitenzi zafanana na maswali ambayo yataulizwa kuhusu tukio. Kwa mfano; nani alifanya nini na alimfanyia nani na lini?

b) Kauli tendi na tendwa hutumia uwakilisho mmoja.

Umbo tendi limeonyeshwa katika sehemu ya juu ya mchoro wa uwakilisho ilhali umbo tendwa limeonyeshwa sehemu ya chini ya mchoro wa uwakilisho. Sifa hii ni mkabala na matokeo ambayo ni adimu kukumbuka muundo kamili wa sentensi kisintaksia ilhali hukumbuka ujumbe muhimu ubebwao na sentensi hiyo.

### 1.7.1 Mihimili ya Nadharia ya Uhusika

Nadharia hii imejengeka katika mihimili mitatu mikuu ambayo ni;

a. Utambuzi wa muundo wa kimsingi wa sentensi ni muhimu kwani hutambulisha mahusiano ya kiuhusika.

Mhimili huu umetumika kuzalisha muundo ndani wa vichwa vya habari za siasa teule.

b. Kanuni uhusika chujaji hutumika kuweka uhusika kwa kila kirai nomino wazi cha lugha.

Mhimili huu umemwongoza mtafiti kutia uhusika faafu katika virai nomino lengwa vya vichwa vya habari za siasa teule.

c. Uhusika huangazia mahusiano ya ndani ya kisemantiki.

Huu ni mhimili ambao umemwongoza mtafiti kufasiri dhima ya maneno katika vichwa vya habari za siasa teule.

### 1.7.2 Aina za Uhusika

Fillmore (1968) amebainisha na kueleza aina saba za uhusika kama ifuatavyo;

a) Uhusika kiima

Hii ni aina ya uhusika ambao umbo la uhusika huwekwa kwenye nomino au kiwakilishi kuashiria kuwa nomino au kiwakilishi hicho ni kiima katika sentensi. Kwa mfano; <u>Rais</u> ateua baraza la mawaziri.

b) Uhusika yambwa

Hii ni aina ya uhusika ambapo umbo la uhusika huwekwa kwenye nomino au kiwakilishi ili kuonyesha kuwa nomino au kiwakilishi hicho ni yambwa katika sentensi. Kwa mfano; Wanafunzi watanunuliwa vipakatalishi.

c) Uhusika tendea

Hili ni umbo la uhusika ambalo huonyesha yule anayeathiriwa na jambo fulani. Kwa mfano; Janga la ufisadi lamkera rais.

d) Uhusika ala

Huu ni uhusika ambao huonyesha kifaa kilichotumika katika utekelezaji wa kitendo au jambo fulani. Kifaa hicho hutumika katika kusababisha utokeaji wa tendo au hali ambayo inadokezwa na kitenzi. Kwa mfano; Mwizi alifungwa kwa pingu.

e) Uhusika mahali

Hili ni umbo la uhusika ambalo huonyesha mahali tendo lilipofanyika. Kwa mfano; Mbunge amesimama jukwaani.

f) Uhusika tokeo

Hili ni umbo la uhusika ambalo hubainisha matokeo au zao la mwisho la kitendo. Kwa mfano; Tume ya maridhiano yawasilisha ripoti ya maridhiano kwa rais na kiongozi wa upinzani.

Aina hizi za uhusika zimemwongoza mtafiti kuteua na kuchambua vichwa viteule vya habari za siasa katika gazeti la *Taifa Leo* ili kufanikisha utafiti husika.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imeeleza eneo la utafiti, muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji data, maadili ya utafiti, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

#### 1.8.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyiwa maktabani. Mtafiti amesoma magazeti ya *Taifa Leo* yaliyoandikwa na kuchapishwa kati ya mwaka wa 2017 na 2019, vitabu na tasnifu za awali zinazohusiana na mada ya utafiti. Makala ya mtandaoni yanayohusiana na suala linalotafitiwa yamesomwa na kutumika katika utekelezaji wa utafiti husika. Nyenzo hizi zote za maarifa zimemsaidia mtafiti kuelewa zaidi eneo lake la usomi na utafiti. Pia, usomaji wa maktabani umemwezesha mtafiti kudhibiti ubora zaidi wa taarifa za kinadharia kuihusu mada husika na kuuwekea utafiti huo misingi.

#### 1.8.2 Muundo wa Utafiti

Mtindo wa michoro ya kisintaksia, majedwali na maelezo umefafanua data kulingana na malengo ya utafiti. Michoroti ya kisintaksia imetumika kuunda na kuchanganua muundo wa ndani wa vichwa vya habari za siasa ndipo kubainisha jinsi kanuni tatu kuu za uwekaji uhusika kwa mujibu wa Fillmore (1968), hutenda kazi. Pia, dhima ya maneno katika vichwa hivyo vya habari imebainishwa huku tofauti kati ya majukumu na maumbo ya uhusika ikiwekwa dhahiri kwa matumizi

ya majedwali. Maelezo mafupi ya ufafanuzi yameandamana na michoroti hiyo pamoja na majedwali ndipo kuweka wazi maana ibebwayo na uchanganuzi huo. Umuhimu wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu umewasilishwa kwa njia ya maelezo.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Kulingana na Kimalu na Marimba (2014), sampuli ni kundi ndogo la watu binafsi, matukio au vitu ambavyo hupatikana katika idadi halisi ya utafiti inayofikika. Kila mwanajumuiya katika sampuli hiyo hujulikana kama mhusika. Katika utafiti huu, vichwa vya habari thelathini ambavyo vimetawaliwa na kigezo cha siasa katika machapisho anuwai ya gazeti la *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya mwaka 2017 na 2019 vimetumika kama sampuli. Sampuli hutumika katika utafiti kwa sababu ya mtafiti kutokuwa na uwezo wa kushughulikia idadi inayofikika kwenye utafiti huo.

Mchakato wa usampulishaji kimakusudi umeongoza suala nzima la uteuzi wa sampuli katika utafiti husika. Kwa mujibu wa Mugenda (2013), sampuli kimakusudi ni aina ya sampuli ambayo humruhusu mtafiti kuchagua wanajumuiya wenye sifa bia na ambao watampa data ambayo anakusudia kukusanya kulingana na malengo ya utafiti wake. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia sampuli ya kimakusudi kuteua magazeti teule ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya mwaka wa 2017 na 2019. Kigezo cha siasa kimemwongoza mtafiti kusampulisha kimakusudi vichwa thelathini vya habari za siasa ndipo kupata data yenye sifa sawia. Uchambuzi wa vichwa vya habari za siasa umefanywa kulingana na aina ya

uhusika, ambapo, katika kila aina ya uhusika vichwa vitano vya habari za siasa vimeorodheshwa. Kati ya vichwa hivyo vitano, kichwa kimoja kitachambuliwa kulingana na kanuni za uwekaji uhusika za Fillmore (1968), ndipo kubainisha jinsi uhusika hutiwa katika sentensi. Miaka ya 2017 na 2018 imehusisha orodha ya vichwa viwiliviwili mtawalia ilhali mwaka wa 2019 umeorodhesha kichwa kimoja. Sababu kuu ya kuteua vichwa viwiliviwili vya habari za siasa kati ya mwaka wa 2017 na 2018 ni kuwa, hii ni miaka iliyotawaliwa na joto jingi mno la kisiasa kinyume na mwaka wa 2019 ambapo, joto lake lilitulizwa na hatua ya kuridhiana kati ya rais na kiongozi wa upinzani.

### 1.8.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Kwa kuwa utafiti huu ni wa maktabani pekee, mtafiti ametumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo katika ukusanyaji wa data yake. Pia, mtafiti amesoma kwa kina magazeti teule ya *Taifa Leo*, yaliyochapishwa kati ya mwaka wa 2017 na 2019 kisha akabainisha sentensi zinazopatikana katika magazeti hayo kama vijianuani vya habari za siasa katika magazeti ya *Taifa Leo*. Vijianuani hivi vya habari za kisiasa ndivyo vilivyotumika kama data ya utafiti.

### 1.8.5 Maadili ya Utafiti

Mtafiti amepata kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, *NACOSTI* ndipo kuutekeleza utafiti wake. Vibali hivi vimemsaidia mtafiti kujitambulisha kwa wepesi na kukusanya data yake bila changamoto yoyote.

Kwa mujibu wa Kimalu na Marimba (2014), wizi wa maandishi ni kosa la jinai katika masuala ya kiakademia. Wizi wa maandishi huhusisha matumizi ya kazi au maarifa ya kiakademia ya mtu mwingine bila kumrejelea. Utafiti huu umezingatia maadili kwa kuhakikisha kuwa kazi inayoandikwa na kuchapishwa ni kazi asili ya mtafiti bali si wizi wa maarifa wala maandishi ya mtu mwingine yule. Maadili mengine yaliyofuatwa ni kuwa; pesa za gharama ya utafiti zilizozotengwa kwa ajili ya utafiti huu zimetumika ipasavyo bila ufisadi wowote. Pia, matokeo ya utafiti huu yamewekwa wazi bila mapendeleo yoyote.

### 1.8.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data umemsaidia mtafiti kuifafanua data yake kwa ajili ya kuwezesha uelewevu kwa watakaoupitia utafiti wake. Mada za kisiasa zilizokusanywa kutoka kwa gazeti la *Taifa Leo* zimepangwa na kuainishwa katika makundi tofautitofauti kulingana na dhana mbalimbali za uhusika ndipo kubainisha mahusiano ya ndani kisemantiki. Majukumu na maumbo ya uhusika yameonyeshwa kwa kuorodheshwa huku kila jukumu likitenganishwa na umbo lake. Umuhimu wa sarufi uhusika katika isimu umetajwa na kuelezwa kwa ukamilifu na utoshelevu. Kwa jumla ni uchanganuzi wa data unaolenga kujibu maswali ya utafiti.

### 1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya uchanganuzi wa data yamewasilishwa kwa njia ya maelezo yanayojumuisha matumizi ya majedwali na maelezo. Majedwali yametumika kuwasilisha matokeo ya aina mbalimbali za dhana ya uhusika na kutenganisha

majukumu na maumbo ya uhusika. Maelezo mafupi kuhusu majedwali haya yametolewa ndipo kufafanua kwa uwazi data iliyowasilishwa. Umuhimu wa sarufi uhusika katika isimu umewasilishwa kwa maelezo kamilifu na toshelevu.

### 1.9 Hitimisho

Sura ya kwanza imetambulisha mada ya utafiti ambayo ni uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Hii ni sura iliyofafanua uhusika kuwa dhana muhimu kisarufi katika uchambuzi wa tungo kwani hutumiwa kuonyesha dhima ya maneno katika tungo hizo. Katika sura hiyo, magazeti ya *Taifa Leo* yaliyochapishwa kati ya mwaka wa 2017 hadi 2019 na mada teule za kisiasa zilibainishwa kuwa upeo na mipaka ya utafiti husika. Tafiti za awali za kifasihi na kiisimu zilizotekelezwa na watafiti kama vile, Naswa (2003), Nyongesa (2005), Karichia (2012) na King'ori (2015) zilitumika kama marejeleo ya maarifa ya masuala yanayohusu magazeti na vipengele vya kifasihi na kiisimu vinavyooana na mada ya utafiti. Msingi wa nadharia ya uhusika iliyoasisiwa na Fillmore (1968) ulielezwa kwa utoshelevu huku mihimili yake ikiorodheshwa kwa umakinifu na ukamilifu. Aina saba za uhusika zilibainishwa huku mtafiti akitoa maelezo mafupi kuzihusu.

# SURA YA PILI

# UHUSIKA KATIKA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA

## 2.1 Utangulizi

Hii ni sura inayodhihirisha dhana mbalimbali za uhusika na jinsi zinavyojitokeza katika vichwa vya habari za siasa zilizoko kwenye magazeti teule ya *Taifa Leo.* Katika kila dhana ya uhusika, vichwa vitano vya habari vimeorodheshwa kama mifano ya sentensi zilizo na uhusika teule. Kichwa kimoja cha habari kati ya vitano vilivyoorodheshwa kimechambuliwa kwa niaba ya vichwa vingine ndipo kuonyesha jinsi uhusika hujitokeza. Kwa mujibu wa Chomsky (1965), kila sentensi katika lugha huwa na kategoria mbili za uwakilisho, ambazo ni muundo ndani na muundo nje. Muundo ndani huwakilisha mahusiano msingi ya kisemantiki katika sentensi huku muundo nje ukiwakilisha umbo la kifonolojia la sentensi hiyo. Nadharia ya uhusika ya Fillmore (1968) ambayo imechambua vichwa vya habari teule imejikita mno kwenye kategoria ya uwakilisho wa muundo ndani wa sentensi.

Vichwa vilivyoko katika magazeti teule ya *Taifa Leo* vimewasilishwa kwa muundo wa nje. Fillmore (1968) amebainisha mfumo wa modeli ya uhusika na kanuni tatu kuu za utiaji uhusika katika sentensi. Mfumo huu wa modeli ya utiaji uhusika na kanuni hizi ndio uliotuongoza katika uundaji wa muundo ndani wa vichwa teule vya habari pamoja na utiaji uhusika faafu kwa vichwa hivyo.

### 2.1.1 Uhusika Kiima

Uhusika kiima ni mojawapo ya aina sita za uhusika alizobainisha Fillmore (1968). Katika data teule ya utafiti, mtafiti ameambatisha mada tano za kisiasa zenye muundo uhusika kiima kwa ajili ya uchambuzi. Kwa mujibu wa Fillmore (1968), nomino au kiwakilishi kinapotumika kama kiima cha kitenzi, hutambulishwa kuwa uhusika kiima. Huu ni uhusika ambao hujibu swali; ni nani aliyetenda kitendo fulani? Hivyo basi, uhusika huu huhusisha vitu vyenye uhai ambavyo husisimua utendaji wa tendo. Kando na kuhusisha viumbe hai pekee, *roboti* na *taifa* hujumuishwa kwenye uhusika kiima kwani ni vitu vyenye uwezo wa kutenda kitendo ambacho kiumbe hai chaweza kutenda.

Muundo wa baadhi ya vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo* ni wa uhusika kiima. Maneno yaliyopigiwa mstari katika vichwa hivi ndiyo hubainisha uwepo wa uhusika kiima kama ifuatavyo;


a) Musila ajiondoa Wiper baada ya kushindwa katika mchujo.
b) Karua asukumwa kuondoa kesi yake dhidi ya Waiguru.
c) Mawaziri 13 watemwa na Uhuru.
d) Sitangatangi, Ruto ajitetea.
e) Raila akemea Matiang’i.

Kielelezo kifuatacho kimekichambua kichwa cha habari; Mawaziri 13 watemwa na *Uhuru* ndipo kuthibitisha jinsi mtenda wa kitendo huwa nguzo kuu katika utiaji

uhusika kiima kwa sentensi. Lengo kuu la mchoroti huu ni kujibu swali, ni nani aliyewatema mawaziri 13?

**Kielelezo 2.1a: Muundo wa uhusika kiima**

Mawaziri 13 watemwa na Uhuru




-Tukio lilikuwa gani?

- *Ni nani alitenda kitendo?*

- Ni nani alitendewa kitendo?

- Kitendo kilitendwa lini?

Katika kielelezo hiki, fahiwa ya kitenzi *tema* imeashiria uwepo wa seti ya uhusika. Uwepo wa seti hii ya uhusika ni ishara ya usahihi wa sentensi kisarufi. Aina za uhusika zinazohusishwa na kitenzi *tema* katika kielelezo hiki zinafanana na maswali ulizwa kuhusu tukio. Kwa mfano; swali, *ni nani alitenda kitendo?* laashiria mtenda wa tukio. Tukio la kutema mawaziri 13 latendwa na *Uhuru*. Hivyo basi, neno *Uhuru* ni uhusika kiima katika kichwa cha habari teule.

**Kielelezo 2.1b: Utiaji uhusika kiima**

a) Muundo nje




Kulingana na Massamba (2012), baada ya kuandika au kutamka maneno, umbo la nje la neno hilo hujitokeza. Muundo nje wa vichwa teule vya habari za siasa hujitokeza zisomwapo. Vichwa hivi vya habari huashiria jinsi vipashio mbalimbali vya lugha huungana na kuunda sentensi kamili na sahihi kisintaksia. Maana ibebwayo na sentensi hiyo hutokana na muundo wake wa ndani.

b) Muundo ndani

Kwa mujibu wa Fillmore (1968), umbo la ndani la sentensi ni dhahania na ndilo kigezo kikuu cha maumbo na miundo yote ya lugha asilia ya binadamu. Kwa hivyo, umbo la ndani hujengeka tu akilini na ndilo hubeba maana ya neno, hivyo ndilo maana. Ufuatao ni muundo ndani wa kichwa cha habari, *Mawaziri 13 watemwa na Uhuru*. Lengo kuu la muundo ndani wa kichwa cha habari teule ni kudondoa maana ibebwayo na vipashio vya lugha viundavyo kichwa hicho.


Uhuru/ atema/ Mawaziri 13

KIM (kiima) T (kitenzi) YA (yambwa)

Katika muundo huu, kila neno hubeba maana kama ilivyoashiriwa kwa michoroti. Hata hivyo, lengo kuu la sura hii ni kutambua aina mbalimbali za uhusika kwa kuzingatia miundo ya vichwa teule vya habari za siasa. Katika mfano huu, inabainika wazi kuwa, neno *Uhuru* ni uhusika kiima kwa kichwa cha habari teule.

Uchambuzi wa mchoroti ufuatao huonyesha jinsi kanuni tatu kuu za utiaji uhusika zake Fillmore (1968) hutenda kazi. Mtafiti anaonyesha wazi kuwa, kichwa hiki cha habari kimeundwa kwa sehemu mbili kuu, nazo ni: kauli na hali. Sehemu ya hali imehusisha kigezo cha wakati pekee; ambao ni wakati uliopo ilhali sehemu ya kauli imehusisha: kitenzi kikuu na mfuatano wa dhana za uhusika mbalimbali kama vile; uhusika yambwa, uhusika mahali na uhusika kiima. Ndipo uhusika utiwe katika sentensi, ishara za uhusika hutanguliza kirai nomino kama inavyoonyeshwa katika mchoroti huu na kanuni ya tatu.

**Mchoroti 2.1: Muundo wa uhusika kiima**




$S \rightarrow KL+HL$

$KL \rightarrow T+UH+UH_n$

$UH \rightarrow K+KN$

Katika uhusika huu, kiima cha kitenzi hukubaliana kwa idadi na nafsi. Kutokana na uchambuzi wa muundo ndani wa kichwa cha habari husika, ni wazi kuwa, kitenzi *tema* chakubaliana na kiima *Uhuru* katika kichwa hicho. Hivyo basi, neno *Uhuru* ni uhusika kiima katika kichwa cha habari teule. Hiyo ndiyo sababu nomino, *Uhuru* itahama mahali ilipo katika muundo wa ndani ili kwenda kabla ya kitenzi hicho kupewa uhusika unaostahili. Fillmore (1968) anasema kuwa, uhusika kiima huhusisha vitu vyenye uhai ambavyo husisimua utendaji wa tendo. Pia, maelezo haya ni ithibati kuwa neno *Uhuru* ndilo linalosisimua tendo la kuachisha kazi mawaziri 13. Neno, *Uhuru* ni jina la mtu na lina uhai, hivyo basi ni uhusika kiima katika kichwa cha habari teule.

Uchambuzi huu hurahisisha mchakato wa kuelewa mada husika na makala yanayoihusu kwa msomaji. Kwa kuongozwa na kauli, ni nani aliyetenda tendo fulani, wasomi mbalimbali wa magazeti huwa na fasiri sawia kinyume na wanaotegemea fasihi katika ufasiri wao. Hivyo basi, ujumbe sawia na faafu huwafikia watu mbalimbali kando na fasiri za kifasihi ambapo, kila msomaji huwa na uhuru wa kusoma kichwa cha makala na kukifasiri kulingana na uelewevu wake.

### 2.1.2 Uhusika Mahali

Uhusika mahali ni mojawapo wa aina sita za uhusika zilizoko kwenye data ya utafiti. Kulingana na Collins (2012), uhusika mahali ni umbo la uhusika ambalo huonyesha mahali ambapo tendo lilifanyika. Vifuatavyo ni baadhi ya vichwa vya habari za siasa ambavyo muundo wake una uhusika mahali.

a) Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura.

b) Viongozi wa ukambani wakutana na rais ikulu.

c) Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini.


d) Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa.

e) Viongozi wamtaka Jumwa ang'olewe uongozini.

Muundo wa uhusika mahali hujibu swali; tukio lilitukia wapi? Kigezo cha mahali ambapo kitendo kilitendeka huongoza mchakato mzima wa muundo wa uhusika. Kichwa kifuatacho cha habari kimechambuliwa ndipo kuwakilisha mchakato mzima wa muundo wa uhusika mahali; *Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini*. Tukio lenyewe ni, *wakilisha* ilhali mahali pa tukio kutendekea ni *mazishini*. Hivyo basi, neno *mazishini* ni uhusika mahali katika muundo ufuatao.

**Kielelezo 2.2a: Muundo wa uhusika mahali**

Raila aenda kuwakilisha nchi *mazishini*




Nchi yawakilishwa na Raila *mazishini*

Hata ingawa kuna seti mbalimbali za uhusika katika kielelezo hiki, kama vile, uhusika kiima, yambwa na mahali, anwani yake imelenga ubainishaji wa muundo

wa uhusika mahali pekee. Maswali yaliyoko kwa mkono wa kulia isipokuwa swali la wakati tendo lilitendeka yanabainisha seti mbalimbali za uhusika zilizoko kwenye fahiwa ya kitenzi, *wakilisha*. Swali la *kitendo kilitendekea wapi* laashiria mahali ambapo tukio lilifanyika. Hivyo basi, neno *mazishini* ni uhusika mahali katika kielelezo hiki.

**Kielelezo 2.2b: Utiaji uhusika mahali**

a) Muundo nje




Picha hii imewakilisha muundo nje wa mojawapo ya data teule iliyokusudiwa kuchambuliwa kwa ajili ya kubainisha uhusika mahali. Kutokana na muundo huu, mtafiti ameunda muundo ndani wa kichwa cha habari teule kwa ajili ya kubainisha ujumbe ubebwao na kichwa hicho.

b) Muundo ndani


Vipashio vyote vya lugha vinavyoungana na kuunda kichwa cha habari teule vimepewa maana. Neno *nchi* lina maana tendea ilhali kitenzi ni *yawakilishwa*. Kihusishi *na* ni ishara uhusika huku neno *Raila* likiwa na maana ya uhusika kiima. Neno, *mazishini* laashiria uhusika mahali.

Nchi/ yawakilishwa/ na/ Raila / mazishini

TD (tendea) T K KIM MH (mahali)

Mchoroti wa muundo wa ndani wa kichwa cha habari teule ufuatao unathibitisha jinsi kanuni tatu kuu za utiaji uhusika katika sentensi hutenda kazi. Katika kanuni ya kwanza, kichwa hiki cha habari kimeundwa kwa sehemu ya hali ambayo imehusisha kigezo cha wakati uliopo na sehemu ya kauli iliyohusisha kitenzi kikuu na mfuatano wa dhana za uhusika. Kanuni ya pili imebainisha kitenzi kikuu kuwa neno *wakilisha* huku mfuatano wa dhana za uhusika yambwa, kiima na mahali ukikiandama kitenzi hicho. Kulingana na Fillmore (1968), uhusika unapotiwa katika sentensi, ishara uhusika hutanguliza kirai nomino kama inavyobainishwa na kanuni kwenye mchoroti.

**Mchoroti 2.2: Utiaji uhusika mahali**




Kigezo cha mahali kitendo kilifanyika ndicho huongoza mchakato mzima wa utiaji uhusika kwa aina hii ya uhusika. Tendo kuu husika katika kichwa cha habari teule ni *wakilisha*. Mtendaji amelitendea tendo hilo *mazishini*. Hivyo basi,

mahusiano ya moja kwa moja kati ya kitenzi na nomino ya kawaida inayoashiria mahali hubainisha uwepo wa uhusika mahali katika sentensi. Mahusiano haya hurahisisha utiaji wa uhusika mahali katika sentensi. Hivyo basi, neno *mazishini*, hubakia kuwa uhusika mahali katika kichwa teule cha habari.

Msomi wa gazeti la *Taifa Leo* anayefahamu vyema jinsi ya utiaji uhusika katika sentensi huwa ni mwepesi wa kuelewa kinachozungumziwa na mwandishi wa makala kwa kukisoma kichwa cha habari pekee. Ufasiri wa kisarufi hujikita kwa kigezo, mahali tendo lilitendeka. Hivyo basi, kigezo hiki huibua usawia katika ufasiri wa maana katika makala teule kwa wasomi wote. Jambo hili hupiga teke fununu ambazo hupitishwa na wasomi wa gazeti ambao huifasiri kwa mapendeleo kwa ajili ya kujifaidi au kusifia mlengo fulani wa kisiasa.

### 2.1.3 Uhusika Yambwa

Uhusika yambwa ni aina nyingine ya uhusika aliobainisha Fillmore (1968). Huu ni uhusika ambao umbo lake la uhusika huwekwa kwenye nomino au kiwakilishi chake ili kuonyesha kwamba nomino au kiwakilishi hicho ni yambwa katika sentensi**.** Kwa ufupi, ni nomino au kiwakilishi kinachopokea pigo katika sentensi.

a) Sitaunga mtu yeyote kwa urais gavana Ruto asema.

b) Akashifu UhuRuto kwa mauaji.

c) Ahadi kuu ya rais iwe ni kuliunganisha taifa.


d) Ruto atetewa kuhusu 2022.

e) Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani.

Kwa kurejelea kichwa cha habari; *Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani*, muundo wa uhusika yambwa unalenga kubainisha neno *mwanawe Too* kama neno linalopokea pigo katika kichwa hicho. Ufuatao ni mchoroti wa uchambuzi unaowakilisha muundo wa aina hii ya uhusika.

**Kielelezo 2.3a: Muundo wa uhusika yambwa**

Chama cha Jubilee chateua *mwanawe Too* kuwa diwani




*Mwanawe Too* ateuliwa na chama cha Jubilee kuwa diwani

Fahiwa ya kitenzi, *teua* ina seti zifuatazo za uhusika; uhusika kiima, uhusika yambwa na uhusika tokeo. Hata hivyo, kwa sababu muundo wa uhusika uliopo ulilenga kubainisha uhusika yambwa, mtafiti aliongozwa na swali kuhusu mpokezi wa pigo la tukio ndipo kubainisha neno *mwanawe Too* kuwa uhusika yambwa. Katika mchoroti huu, kauli tendi na tendwa zimetumia uwakilisho mmoja kama inavyoonekana. Uwakilisho huo humsaidia msomi kukumbuka ujumbe ubebwao na kichwa cha habari teule.

**Kielelezo 2.3b: Utiaji uhusika yambwa**

a) Muundo nje



Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani

Na DENNIS LUBANGA

UASIN GISHU

4/9/2019

Kichwa cha habari kilichoko kwenye picha ya gazeti iliyotangulia maelezo haya huwakilisha yale maoni ya mwandishi baada ya kufanyiwa mabadiliko. Kutokana na muundo huu, mtafiti amebuni muundo ndani wake kwa ajili ya kudondoa maana ifungamanayo na kichwa hiki.

b) Muundo ndani


Kila kipashio kiundacho muundo ndani wa kichwa cha habari teule kina dhima yake. Neno, *mwanawe Too* lina dhima ya uhusika yambwa huku kitenzi kikuu

kikiwa neno *ateuliwa.* Kipashio, *chama cha Jubilee* kimepewa maana, uhusika kiima ilhali neno *diwani* lina dhima ya uhusika tokeo. Namna ya utiaji uhusika katika muundo huu umelenga kwa uhusika yambwa kama itakavyoonyeshwa katika mchoroti wa muundo ndani ufuatao.

| Mwanawe Too/ | ateuliwa/ | na/ | chama cha Jubilee/ | kuwa/ | diwani |
|---|---|---|---|---|---|
| YA | T | K | KIM | K | TK (tokeo) |

Kichwa cha habari, *mwanawe Too ateuliwa na chama cha Jubilee kuwa diwani* kimegawanywa kwa sehemu mbili kuu: sehemu ya hali, ambayo inahusisha kigezo cha wakati uliopo na sehemu ya kauli ambayo inahusisha kitenzi kikuu na mfuatano wa dhana mbalimbali za uhusika. Kitenzi kikuu katika sehemu ya kauli ni *ateuliwa* ilhali aina za uhusika unaofuatana ni pamoja na; uhusika yambwa, uhusika kiima na uhusika tokeo. Ishara kapa ya uhusika imetanguliza kirai nomino *mwanawe Too* katika utiaji uhusika yambwa kwenye muundo huu wa uhusika kama inavyodhihirishwa. Mtafiti amezingatia utendakazi wa kanuni tatu kuu za utiaji uhusika zake Fillmore (1968) alizobainisha katika modeli yake ya mfumo wa uhusika kama ilivyo katika mchoroti ufuatao.

**Mchoroti 2.3: Utiaji uhusika yambwa**




Neno linalopokea pigo katika kichwa hiki cha habari ni *Mwanawe Too*. Hivyo basi, hili ndilo neno lililo na uhusika yambwa kwa mujibu wa maelezo ya Fillmore (1968) kuhusu dhana ya uhusika yambwa.

Kwa kufahamu dhana ya uhusika, wasomi wa gazeti huongozwa na kauli, ni nani aliyepokea pigo la kitendo fulani. Kauli hii huleta usawa wa maana kisemantiki kutoka kwa msomi mmoja hadi mwingine kwani, mahusiano kati ya kitenzi kikuu na yambwa huwa wazi. Jambo hili husababisha upitishaji wa taarifa sawia za habari kwa wananchi na kuondoa utata wa fasili mbalimbali za kichwa kimoja.

### 2.1.4 Uhusika Tendea

Hili ni umbo la uhusika ambalo huonyesha mhusika anayeathiriwa na jambo fulani. Baadhi ya vichwa teule vya habari vilivyoko katika gazeti la *Taifa Leo* vyenye uhusika tendea ni kama ifuatavyo;

a) Wezi waburudika kabla kuibia mwanasiasa.

b) Uamuzi wa Kanu kutoteua mwaniaji wakanganya na kuwa mgawanyiko.

c) Uhuruto wamefanya nifilisike, afichua Joho.


d) Si ustaarabu wanasiasa kutimua *walimu wapya*.

e) Uhuru aliteua Nyachae kama njia ya kumzawadi.

Kwa kurejelea kichwa cha habari; *Si ustaarabu wanasiasa kutimua walimu wapya*, athari ya kitendo *timua* hujitokeza kwa maneno *walimu wapya*. Hivyo basi, uhusika tendea katika kichwa hiki upo kwa maneno, *walimu wapya*.

**Kielelezo 2.4a: Muundo wa uhusika tendea**

Si ustaarabu wanasiasa kutimua *walimu wapya*




Si ustaarabu *walimu wapya* kutimuliwa na wanasiasa

Katika kielelezo hiki, uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitenzi, mtenda wa kitendo na mtendewa umeweza kuibua seti ifuatayo ya uhusika: uhusika kiima, *wanasiasa* na uhusika tendea, *walimu wapya*. Hata hivyo, anwani ya muundo huu

wa uhusika imelenga kubainisha uhusika tendea pekee. Uhusika tendea umebainika wazi kwa kuzingatia kigezo cha athari. Kigezo hiki cha athari kimemsaidia mtafiti kujibu swali, *mwathiriwa wa tendo hili ni nani?* Wanaoathiriwa na tendo la kutimuliwa shuleni na wanasiasa ni walimu wapya. Hivyo basi, *walimu wapya* ni uhusika tendea kama ilivyobainishwa katika kielelezo 2.4a.

**Kielelezo 2.4b: Utiaji uhusika tendea**

a) Muundo nje


Jumatatu, Januari 15, 2018 TAIFA LEO

Tunawaonyesha watoto wetu mfano mbaya maishani kwa utundu huu

Si ustaarabu wanasiasa kutimua walimu wapya

15/1/2018

Kichwa hiki cha habari kimetumika kama kielekezo cha kuunda muundo ndani kwa ajili ya uchambuzi na utiaji uhusika.

b) Muundo ndani


Ufuatao ni muundo ndani wa kichwa cha habari, *si ustaarabu wanasiasa kutimua walimu wapya*.

Si/ ustaarabu/ walimu wapya /kutimuliwa /na/ wanasiasa
| | | | | |
ts TK TD T K KIM

Katika muundo huu, kila neno lina dhima yake. Kwa mfano; *si* ni kitenzi kishirikishi kipungufu, *ustaarabu* ni uhusika tokeo, *walimu wapya* ni uhusika tendea, *kutimuliwa* ni kitenzi kikuu, *na* ni ishara uhusika na *wanasiasa* ni uhusika kiima.

Uchambuzi wa muundo ndani ufuatao umeangazia jinsi uhusika tendea hutiwa katika vichwa vya habari za siasa. Utiaji uhusika tendea huu umeongozwa na kanuni tatu kuu za utiaji uhusika zilizoasisiwa na Fillmore (1968). Kanuni ya kwanza imekigawa kichwa cha habari kwa sehemu mbili kuu, ambazo ni: kauli na hali. Sehemu ya hali ina kigezo cha wakati uliopo pekee ilhali sehemu ya kauli ina kigezo cha kitenzi na mfuatano wa aina mbalimbali za uhusika. Kitenzi kikuu *timua* kimeandamana na kitenzi kishirikishi kipungufu *si*, aina mbalimbali za uhusika kama vile; uhusika tokeo, uhusika tendea na uhusika kiima. Kila aina ya uhusika imetangulizwa na ishara ya uhusika ambayo huonyesha kirai nomino ambacho chafaa kutiliwa uhusika. Kwa kutolea mfano; kirai nomino, *walimu wapya*, ambacho kimepewa maana ya uhusika tendea kimetangulizwa na ishara kapa ya uhusika.

**Mchoroti 2.4: Utiaji uhusika tendea**




Fillmore (1968) anasema kuwa, uhusika tendea huhusisha uhusiano usiokuwa wa moja kwa moja kati ya yambwa katika sentensi na kitenzi. Kutokana na maelezo haya, uhusika tendea katika kichwa hiki cha habari, hutukia kwa neno *walimu wapya*.

Usawia wa kimaana kwa wasomi wa magazeti huongozwa na kigezo cha neno lililopokea pigo. Kisarufi, dhana ya uhusika yambwa hufafanua wazi uhusiano uliopo kati ya kitenzi na yambwa katika sentensi, hivyo basi, mahusiano haya huleta uelewevu bia kwa wasomi wote hivyo kuondoa utata wa kimaana.

### 2.1.5 Uhusika Tokeo

Mtafiti alibaini uhusika tokeo kama aina nyingine ya uhusika alioupata kwa data yake. Uhusika tokeo ni umbo la uhusika ambalo hubainisha matokeo au zao la

mwisho la kitendo. Vifuatavyo ni baadhi ya vichwa teule vya habari za siasa vilivyoko katika gazeti la *Taifa Leo*;

a) Wapwani wabuni muungano wao

b) Mudavadi kuongoza kampeni za NASA

c) Miguna ageuzwa kipenzi cha Raila


d) Misururu ya kashfa haimbanduki Keter

e) Tangatanga yadai wakuu walileta fujo

Maneno yaliyopigiwa mstari katika vichwa teule vya habari huwakilisha dhana ya uhusika tokeo. Kwa kurejelea kichwa cha habari; *Wapwani wabuni muungano wao*, neno *muungano wao* ndio zao la mwisho la kitendo *buni*. Muundo wa uhusika tokeo katika mchoroti huwakilishwa kama ifuatavyo;

**Kielelezo 2.5a: Muundo wa uhusika tokeo**

Wapwani wabuni *muungano wao*




*Muungano wa wapwani* wabuniwa

Uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitenzi *buni* na mtenda, *wapwani* au tokeo, *muungano wao* umeibua uwepo wa seti ya uhusika ambayo ni: uhusika ni kiima na uhusika tokeo mtawalia. Hata hivyo, anwani ya muundo huu wa uhusika imelenga kubainisha uhusika tokeo kati ya aina nyinginezo za uhusika. Kwa kuzingatia kigezo cha zao la mwisho la tendo, jibu la swali, *ni nini zao la mwisho la tendo* ndilo uhusika tokeo kama ilivyobainishwa katika muundo huu. Jibu hilo ni *muungano wao*. Hivyo basi, *muungano wao* ni uhusika tokeo katika kichwa teule cha habari.

**Kielelezo 2.5b: Utiaji uhusika tokeo**

a) Muundo nje


Wasema nia ni kuzuia mshindi katika raundi ya kwanza kwenye uchaguzi ujao

Wapwani wabuni muungano wao

20/2/2017

Kichwa hiki cha habari ni mojawapo ya data teule ya kubuniwa muundo ndani. Muundo nje wa kichwa hiki unaashiria yale mawazo ya tendo baada ya kuandikwa. Kisintaksia, huu ni muundo ambao umewasilisha sentensi sahihi na kamilifu kisarufi.

b) Muundo ndani

<u>Muungano wa Wapwani</u> <u>wabuniwa</u>


TK T

Muundo ndani wa kichwa cha habari teule umeundwa kwa vipashio viwili. Kipashio cha kwanza ambacho ni *muungano wa wapwani* kina uhusika tokeo ilhali kipashio cha pili, *wabuniwa* ndicho kitenzi kikuu katika kichwa cha habari teule.

Kichwa cha habari, *Muungano wa wapwani wabuniwa* kimegawanywa katika sehemu mbili kuu. Sehemu ya kwanza ni hali. Hii ni sehemu iliyotawaliwa na kigezo cha wakati uliopo pekee. Sehemu ya pili ni kauli. Katika sehemu hii,

kitenzi kikuu na mfuatano wa uhusika hutawala. Kitenzi kikuu, *wabuniwa* na uhusika tokeo, *muungano wa wapwani* umethibitisha utendakazi wa kanuni ya pili ya utiaji uhusika. Ishara kapa ya uhusika tokeo imetanguliza kirai nomino, *muungano wa wapwani* ambacho ndicho uhusika tokeo katika kichwa hiki cha habari. Mchoroti ufuatao umethibitisha jinsi uhusika tokeo hutiliwa katika kichwa cha habari za siasa kwa kuzingatia tokeo la mwisho la tendo.

**Mchoroti 2.5: Utiaji uhusika tokeo**




$S \rightarrow KL+HL$

$KL \rightarrow T+UH+UH_n$

$UH \rightarrow K+KN$

Zao la mwisho la uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitenzi, *buni* na nomino, *Wapwani*, ni *muungano wa wapwani*. Tofauti iliyopo kati ya muungano huu na mingine ya kisiasa ni kuwa, muungano huu unamilikiwa na wapwani. Kwa hivyo, ni wazi kuwa, *muungano wa wapwani* ni uhusika tokeo katika kichwa cha habari teule.

Kwa kutambua tokeo la mwisho la kitenzi katika sentensi husika, maana kisemantiki ya sentensi hubainika. Tokeo la mwisho ndilo nguzo kuu katika ufasiri wa maana kisemantiki wa vichwa vya habari teule, hivyo basi, maana sawia hujitokeza wakati wa ufasiri kati ya wasomi. Usawia huu huleta uelewevu unaooana kwa kila mtu, hivyo, kupitisha ujumbe sawia wa habari na kuondoa utata wa ufasiri wa kimaana wa kichwa cha habari teule.

### 2.1.6 Uhusika Ala

Kwa mujibu wa Collins (2012), uhusika ala ni umbo la uhusika ambalo huonyesha kifaa kilichotumika katika utekelezaji wa kitendo au jambo fulani. Kifaa hicho hutumika katika kusababisha utokeaji wa tendo au hali ambayo inadokezwa na kitenzi. Ifuatayo ni mifano ya baadhi ya vichwa vya habari za siasa zenye muundo wa uhusika ala;

a) Mwanafunzi aliuawa kwa risasi.

b) 5 wahofiwa kufa ajali ya helikopta.

c) NASA waache mizaha ya kutumia Bibilia kujiapisha.


d) Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi.

e) Shoka la Obado latia hofu maafisa wakuu.

Muundo wa uhusika ala wa kichwa cha habari; *Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi* umetumika kama mfano ili kuonyesha jinsi uhusika huu hujitokeza katika sentensi. Mchoroti ufuatao unawakilisha maelezo haya

**Kielelezo 2.6a: Muundo wa uhusika ala**

Teknolojia ya blockchain itumiwe kuzima ufisadi




Ufisadi uzimwe kwa *teknolojia ya blockchain*

**Kielelezo 2.6b: Utiaji uhusika ala**

a) Muundo nje


Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi

177/2018

Muundo huu umetumiwa kama kielelezo cha kudondoa muundo ndani wa kichwa cha habari husika ndipo mchakato wa utiaji uhusika katika kichwa hiki ufanikishwe.

b) Muundo ndani

Ufisadi uzimwe kwa teknolojia ya blockchain


YA T K AL

Muundo ndani huu umeundwa kwa vipashio vinne. Kila kipashio kimebeba maana. Neno, *ufisadi* ni yambwa ilhali *uzimwe* ndicho kitenzi kikuu katika kichwa hiki. Kihusishi *kwa* ni ishara ya uhusika ala ilhali *teknolojia ya blockchain* ndiyo imepewa uhusika ala.

Mchoroti wa uchambuzi wa muundo ndani ufuatao umefanikisha utendakazi wa kanuni tatu kuu za utiaji uhusika katika sentensi kwa mujibu wa Fillmore (1968). Maandishi ya mlazo yaliyo upande wa kushoto ndiyo kanuni tatu kuu za utiaji uhusika ilhali uchambuzi ulioko katika michoroti unaashiria jinsi kanuni hizo hutenda kazi. Kanuni ya kwanza imekigawa kichwa cha habari teule katika sehemu mbili kuu ambazo ni hali na kauli. Sehemu ya hali ina kigezo cha wakati uliopo pekee ilhali sehemu ya kauli ina vigezo vya kitenzi kikuu; *uzimwe* na mfuatano wa aina mbili za uhusika; uhusika yambwa na uhusika ala. Hata hivyo, muundo wa uhusika huu umelenga kubainisha utiaji wa uhusika ala katika mchoroti huu. Hivyo basi, kwa kuzingatia kigezo cha ala iliyotumika kutendea kitendo lengo kuu katika mchoroti huu ni kubainisha uhusika ala. Kanuni ya tatu imetumika kuonyesha utambuzi wa uhusika katika sentensi. Katika kanuni hii, ishara ya uhusika imetanguliza kirai nomino kilicho na uhusika lengwa. Kwa

mfano; ishara ya uhusika *kwa* imetanguliza kirai nomino *teknolojia ya blockchain* ambacho ndicho uhusika ala katika kichwa hiki cha habari.

**Mchoroti 2.6: Utiaji uhusika ala**




Tukio linalodhamiriwa kutendwa ni *uzimaji*. Kinachodhamiriwa kuzimwa ni tendo la *ufisadi* nchini Kenya. Kifaa kinachopendekezwa kitumike katika utekelezaji wa tukio hili ni *teknolojia ya blockchain*. Hivyo basi, *teknolojia ya blockchain* ni uhusika ala katika kichwa cha habari husika.

Nguzo kuu katika kubaini uhusika ala ni kujibu swali, ni kifaa gani kilichotekeleza tukio fulani. Msomi wa gazeti anayefahamu jinsi ya kutia uhusika ala katika sentensi huwa mwepesi wa kutambua suala kuu linalokisiwa kuzungumziwa katika makala yote. Ufahamu huu hurahisisha uelewaji wake kuhusu suala linalogusiwa na kuleta fasili moja ya maana kisemantiki katika kichwa cha habari teule.

**2.2 Hitimisho**

Sura ya pili imebainisha dhana sita za uhusika kwa mujibu wa Fillmore (1968). Dhana hizo za uhusika ni pamoja na: uhusika kiima, uhusika mahali, uhusika yambwa, uhusika tendea, uhusika tokeo na uhusika ala. Pia, muundo wa ndani na wa nje wa aina hizi za uhusika umeonyeshwa kwa uwazi. Muundo nje umewakilishwa kwa picha za vichwa vya habari teule vilivyoko katika magazeti ya *Taifa Leo* huku muundo ndani ukiundwa kwa kuzingatia ujumbe ulioko katika picha hizo. Imebainika wazi kuwa, mahusiano kati ya kitenzi na nomino au kiwakilishi chake katika sentensi hubainisha aina ya uhusika.

Kila aina ya uhusika hutambulishwa kwa jibu la swali maalum kama ifuatavyo: jibu la swali, kitendo kilitendwa na nani huwa uhusika kiima ilhali jibu la swali kitendo kilitendewa wapi hubainisha uhusika mahali. Jibu la swali, ni nani aliyepokea pigo katika tukio huwa uhusika yambwa huku uhusika tendea ukibainishwa kwa kigezo cha mwathiriwa wa tendo. Zao la mwisho la tukio linapobainishwa katika sentensi huashiria uhusika tokeo huku kifaa kilichotumika kufanyia tendo kikidhihirisha uwepo wa uhusika ala. Kwa kuzingatia maswali haya, wasomi wa magazeti wataweza kudondoa maana sawia ya vichwa hivyo vya habari na kupunguza utata wa kimaana baina yao. Mfumo wa modeli ya uhusika yake Fillmore (1968) na kanuni tatu kuu za utiaji uhusika, zimeongoza mchakato mzima wa utiaji uhusika kama ilivyothibitishwa katika michoroti.

# SURA YA TATU

# TOFAUTI KATI YA MAJUKUMU NA MAUMBO YA UHUSIKA KATIKA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA

## 3.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, mtafiti amebainisha muundo wa uhusika na jinsi uhusika huo hujitokeza katika vichwa teule vya habari za siasa. Kwa kurejelea muundo huo wa uhusika na namna uhusika huo ulivyojitokeza, tofauti iliyopo kati ya majukumu na maumbo ya uhusika imebainishwa katika sura hii. Tofauti hizi zimegawika katika sehemu sita zifuatazo; tofauti kati ya jukumu mtendi na umbo la uhusika kiima, tofauti kati ya jukumu mahali na umbo la uhusika mahali, tofauti kati ya jukumu mtendwa na umbo la uhusika yambwa, tofauti kati ya jukumu tendea na umbo la uhusika tendea, tofauti kati ya jukumu ala na umbo la uhusika ala na tofauti kati ya jukumu tokeo na umbo la uhusika tokeo. Mawazo ya Fillmore (1968) kuhusu aina sita za uhusika; uhusika kiima, uhusika mahali, uhusika ala, uhusika yambwa, uhusika tendea na uhusika tokeo, yamemwongoza mtafiti kuigawa sura hii katika sehemu sita kuu kando na sehemu ya utangulizi na hitimisho.

## 3.1 Tofauti kati ya Majukumu na Maumbo ya Uhusika

Sehemu hii ya utafiti inahusisha maelezo mapana kuhusu tofauti iliyopo kati ya majukumu na maumbo ya uhusika. Maelezo haya yanatanguliza data ya utafiti iliyotolewa na kuchanganuliwa katika sura hii.

Kwa mujibu wa Fillmore (1968), majukumu ya uhusika huwa na chembechembe za seti bia za kisemantiki ambazo huwa ngumu kubainishwa. Hakuna mbinu kubalifu wala makubaliano kuhusu ubia huo. Aghalabu, huhitaji kutenganishwa kwa kutumia kipimo cha kisemantiki. Hata hivyo, kutambulisha majukumu na upachikaji wa hoja husika katika majukumu huhusisha mgao ziada wa kiisimu wa mahusiano kati ya kitu na ulimwengu.

Kwa mujibu wa Brecht na Levine (1986), ishara uhusika za kimofolojia hutumika kutoa maelezo kuhusu majukumu ya kiuhusika. Maelezo haya huonyesha jinsi mtumizi wa lugha huelewa tukio katika lugha na mahusiano ya tukio hilo na viambajengo vingine katika lugha husika. Campe (1994) anaunga mkono maelezo ya Brecht na Levine (1986) kwa kusema kuwa, kutokana na uzingatifu wa kipengele cha isimu cha sintaksia, majukumu ya uhusika hutokana na mahusiano ya kisintaksia yaliyopo katika vishazi.

Kulingana na Janda (1993), jukumu la kisemantiki hupatikana katika kategoria zote za kisintaksia. Campe (1994) amezitaja baadhi ya kategoria hizo kama ifuatavyo: kiima, kiarifu cha moja kwa moja, kiarifu kisichokuwa cha moja kwa moja, kijalizo na kadhalika. Kutokana na maelezo haya, Fillmore (1968) ametaja majukumu sita ya uhusika kama ifuatavyo: mtendi, mtendwa, mtendea, mahali, tokeo na ala. Mahusiano ya kisemantiki yanayoelezwa kwa mbinu ya mwishio wa kipekee wa kiuhusika katika lugha zenye ishara uhusika dhahiri zimepokea majina sawia na ishara zenyewe. Majina haya: tendea, mahali, tokeo na ala hujitokeza

katika kategoria ya aina mbalimbali za uhusika na kategoria ya majukumu ya uhusika jinsi yalivyo. Jukumu la uhusika kiima ni mtendi huku la yambwa likiwa mtendwa.

Blake (2004) anasema kuwa, uhusika hutawaliwa na kipashio ambacho kisintaksia huungana na kirai ili kuonyesha jinsi ya kukifasiri kirai hicho katika muktadha husika. Kipashio hicho chaweza kuwa kihusishi au kiambishi tamati. Fasiri iibuliwayo kutokana na mahusiano ya kihusishi na kirai nomino au kiambishi tamati na kirai nomino huwa ndilo jukumu katika sentensi teule. Kutokana na ufafanuzi huu ni wazi kuwa, jukumu la uhusika katika sentensi ni dhahania. Naye, Campe (1994) anasema kuwa, utiaji uhusika hutambulishwa na muundo wa kisintaksia wa sentensi. Hivyo basi, kimuundo vitenzi au vihusishi hutumika kutia uhusika katika nomino au kirai nomino. Vivyo hivyo, kutokana na mahusiano ya kitenzi na kirai nomino, jukumu la uhusika hudondolewa.

Kulingana na Blake (2004), maumbo ya uhusika huhusisha namna ya kutoa maelezo kuhusu uhusika teule. Maumbo haya huwa hayabebi maana yoyote bali hutanguliza jukumu la uhusika ambalo ndilo hubeba maana. Campe (1994) akimnukuu Creissels (2005) anasema kwamba, kulingana na maarifa yake hakuna lugha ya Kiafrika ambayo huonyesha hadharani mfumo wa uhusika. Hivyo basi, si jambo la kushangaza la kuwepo kwa unadra wa uhusika na dhana zinazohusiana na uhusika katika isimu ya Kiswahili ya sasa. Pia, kwa kuzingatia hadhi dhahiri ya viambishi kama ishara kubalifu kulingana na utendakazi wake, kipashio cha

kiwakilishi cha nomino hutumika kuashiria umbo la uhusika hata ingawa hakisuluhishi unadra huo. Suala hili hupuuzwa kwa makisio kuwa Kiswahili hakionyeshi hadharani ishara uhusika yoyote kwa viambajengo vya kiima kama asemavyo Krifka (1995). Mfano wa sentensi ifuatayo unadhihirisha wazi maoni ya Krifka (1995): *alikupiga*

*a* (mtendi)-*li* (njeo)-*ku* (mtendwa)-*pig* (kitenzi)-*a* (hali)

Katika sentensi hii, kitenzi kina hoja mbili: hoja ya mtendi na mtendwa. Hoja ya mtendi imebebwa na kiambishi *a* huku hoja ya mtendwa ikibebwa na kiambishi *ku*. Kiambishi *a* (yeye) na kiambishi *ku* (wewe) ni viwakilishi nafsi vya tatu umoja na pili umoja mtawalia. Viambishi hivi vimechukua nafasi ya kirai nomino cha mtendi na mtendwa katika sentensi teule, hivyo basi kuwa, maumbo ya uhusika kiima na yambwa mtawalia. Maelezo haya ndiyo pekee yaliyo na utambuzi wa mfumo wa uhusika katika Kiswahili. Hata hivyo, utofauti huu hutokezea katika muktadha uliowekewa mipaka pekee, ambao ni wenye: kirai nomino katika nafsi ya pili na kirai nomino katika nafsi ya tatu.

Mvati, Maina na Kanuri (2014) wametaja aina kumi na moja za viwakilishi. Aina hizi ni pamoja na; viwakilishi nafsi, viwakilishi vya ngeli, viwakilishi vya ‘a’ unganifu, viwakilishi vimilikishi, viwakilishi viulizi, viwakilishi vionyeshi, viwakilishi virejeshi, viwakilishi vya sifa, viwakilishi vya idadi, viwakilishi vya pekee na viwakilishi visisitizi. Kando na matumizi ya viwakilishi nafsi kama maumbo ya uhusika kwenye virai nomino vya kundi 1/2 kimofolojia, aina hizi nyingine za viwakilishi hutumika kama maumbo ya uhusika kwa virai nomino

visivyokuwa vya kundi la 1/2 kimofolojia. Kiwakilishi faafu kinachofaa sentensi teule huchukua nafasi ya kirai nomino lengwa kama umbo la uhusika. Kisintaksia, ufaafu wa kiwakilishi teule huthibitishwa na usahihi wa sentensi lengwa kisarufi.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa, lugha ya Kiswahili haina maumbo ya kimofolojia ya uhusika, kiasi kidogo kilichobaki ni viambishi nafsi. Viambishi nafsi hivi ndivyo vimetumika kurejelea maumbo ya uhusika katika uchanganuzi wa vichwa vya habari teule. Pale ambapo majina tofauti na kundi la 1/2 kimofolojia yamehusika, mtafiti ametumia viwakilishi husika vya ngeli hizo kurejelea maumbo. Majukumu ya uhusika nayo, hutegemea aina ya uhusika, hivyo basi, kila aina ya uhusika huwa na jukumu lake binafsi. Majukumu haya hutofautiana kutoka uhusika mmoja hadi mwingine kinyume na maumbo ya uhusika (viwakilishi) ambayo ni bia.

### 3.1.1 Tofauti kati ya Jukumu Mtendi na Umbo la Uhusika Kiima

Blake (2004), akirejelea makala ya Fillmore (1968) ya *Case for Case*, anasema kuwa, jukumu mtendi huashiria kitu ambacho hutenda kitendo au kitu ambacho huleta mabadiliko kwa uwepo wa kitu. Jukumu hili hutambulishwa na mahusiano ya moja kwa moja kati ya nomino na kitenzi kikuu. Pia, uwepo wa kihusishi *na* katika muundo wa sentensi hutanguliza sehemu ya sentensi ibebayo jukumu mtendi. Kwa mujibu wa Krifka (1995), umbo la uhusika kiima huwa ni viwakilishi nafsi vya pili, umoja na wingi (*wewe*, *wao*) na tatu, umoja na wingi (*yeye*, *nyinyi*). Kwa kuzingatia usarufi na usahihi wa muundo wa sentensi kisintaksia, kiwakilishi nafsi kimoja kati ya hivi (*wewe*, *wao*, *yeye*, *nyinyi*)

huchukua nafasi ya kirai nomino kilicho na uhusika kiima na kuwa umbo la uhusika lengwa, kama ilivyo katika Jedwali la 3.1.

**Jedwali 3.1: Tofauti kati ya Jukumu Mtendi na Umbo la Uhusika Kiima**

| | **Vichwa teule vya habari** | **Jukumu la uhusika** | **Umbo la uhusika** (Viwakilishi nafsi huchukua nafasi ya kirai nomino lengwa) | **Ufafanuzi wa umbo la uhusika** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Musila ajiondoa Wiper baada ya kushindwa katika mchujo | Mtendi (Musila) | *Yeye* ajiondoa Wiper baada ya kushindwa katika mchujo | *Yeye* ni kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja ( $W.nf._{3u}$) |
| 2 | Karua asukumwa kuondoa kesi dhidi ya Waiguru | Mtendi (Karua) | *Yeye* asukumwa kuondoa kesi dhidi ya Waiguru | *Yeye* ni ( $W.nf._{3u}$) |
| 3 | Mawaziri 13 watemwa na Uhuru | Mtendi (Mawaziri) | *Wao* 13 watemwa na Uhuru | *Wao* ni kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi ( $W.nf._{2w}$) |
| 4 | Sitangatangi, Ruto ajitetea | Mtendi (Ruto) | Sitangatangi, *yeye* ajitetea | *Yeye* ni ( $W.nf._{3u}$) |
| 5 | Raila akemea Matiang’i | Mtendi (Raila) | *Yeye* wamtaka rrais nyumbani | *Yeye* ni ($W.nf._{3u}$) |

Jedwali 3.1 linahusisha vichwa teule vitano vya habari: *Musila ajiondoa Wiper baada ya kushindwa katika mchujo, Karua asukumwa kuondoa kesi dhidi ya Waiguru, Mawaziri 13 watemwa na Uhuru, Sitangatangi, Ruto ajitetea* na *Raila akemea Matiang'i*, ambavyo vimetumika kuonyesha tofauti iliyopo kati ya jukumu mtendi na umbo la uhusika kiima kama inavyoelezwa na mtafiti katika aya inayofuata.

Velten (1964) akinukuliwa na Campe (1994) anasema ya kwamba, Kiswahili hakina nomino hafifu. Hivyo basi, nomino zipatikanazo katika virai nomino vilivyoko katika sentensi huwa na hadhi sawa kiuhusika. Jukumu la uhusika hudondolewa kutokana na aina ya uhusika. Jukumu mtendi hudondolewa kwa uhusika kiima. Hili ni jukumu ambalo hutanguliza kitenzi kikuu. Kiisimu, sentensi hugawika katika sehemu mbili kuu ambazo ni: kiima na prediketa. Kiima ni kirai nomino ambacho prediketa hutoa maelezo kukihusu. Kama kitenzi kikuu katika prediketa ni kitenzi kitendaji hivyo basi, kiima hutambua mtu au kitu kilichofanya kitendo kielezwacho na kitenzi kikuu. Mahusiano kati ya kiima na kiarifu cha moja kwa moja huzindua jukumu mtendi katika sentensi. Maumbo ya uhusika hutokea tu kwenye virai nomino vyenye nafsi ya pili na ya tatu.

Kutokana na mahusiano ya kiarifu cha moja kwa moja na kiima husika katika kila kichwa cha habari; nomino: *Musila*, *Karua*, *mawaziri*, *Ruto* na *Raila* ni ithibati ya jukumu mtendi. Mahusiano haya pia hubainisha kiwakilishi nafsi faafu ambacho huchukua nafasi ya kirai nomino chenye nomino iliyoko katika ngeli ya 1/2

kimofolojia. Maumbo ya uhusika katika vichwa vya habari, *Musila ajiondoa Wiper baada ya kushindwa katika mchujo*, *Karua asukumwa kuondoa kesi dhidi ya Waiguru*, *Sitangatangi*, *Ruto ajitetea* na *Raila amkemea Matiang'i* ni kiwakilishi nafsi cha tatu umoja (*yeye*) ilhali kiwakilishi nafsi cha pili wingi (*wao*) ni umbo la uhusika katika kichwa cha habari, *Mawaziri 13 watemwa na Uhuru*.

Kwa kuzingatia maelezo haya, ni wazi kuwa tofauti iliyopo kati ya jukumu mtendi na umbo la uhusika limewekwa wazi.

### 3.1.2 Tofauti kati ya Jukumu Mahali na Umbo la Uhusika Mahali

Kwa mujibu wa Newmeyer (2010), jukumu hili huashiria mahali kitu kilipo. Bily (1990) akimnukuu Seidel (1988) anasema kuwa, wakati mwingine huwa vigumu kubainisha vipashio hivi vya maumbo ya uhusika katika baadhi ya lugha kwa sababu ya muundo wao wa uhusika. Hivyo basi, katika aina hii ya tukio mahusiano ya kiuhusika hubainishwa moja kwa moja kisemantiki bila kuzingatia maumbo ya uhusika bali mgao ziada wa kiisimu wa mahusiano kati ya kitu na ulimwengu. Neno la kimsingi katika jukumu la uhusika mahali hutangulizwa na kihusishi *kwa* au likahitimishwa na kiambishi tamati *ni*. Hili ni neno ambalo hubeba maana ya mahali kitendo hutendeka. Kihusishi *kwa* na kiambishi tamati –*ni* vina jukumu moja la kuashiria uwepo wa uhusika mahali katika sentensi. Iwapo muundo wa sentensi una kihusishi *kwa*, kabla ya neno linaloashiria mahali kitendo kilitendeka basi, kiambishi tamati *ni* hakijumuishwi popote katika neno hilo. Vivyo hivyo, iwapo neno linaloashiria mahali lina kiambishi tamati *–ni*, basi kihusishi *kwa* huwa hakilitangulizi neno hilo.

Samson na Schadeberg (1994) wakimnukuu Meinhof (1942) wanasema ya kwamba, asili ya kiambishi tamati *ni* ni kiwakilishi kionyeshi cha ngeli ya 18 yenye maana ya undani. Uhusiano huu unaonekana katika neno la zamani sana ambalo ni *nda* lenye maana ya *tumbo* na limetoweka katika Kiswahili. Maelezo haya yanafafanua wazi kuwa, kiambishi tamati *ni* huwa hakijitokezi pahali popote pale bali hujitokeza eneo ambalo huashiria hasa undani wa kitu. Aghalabu kiambishi hiki hujitokeza katika nomino za kawaida ziashiriazo undani wa mahali fulani ambapo undani huwa ni jukumu mahali. Nomino za kipekee zitajazo mahali mahususi hupewa jukumu kwa kuzingatia mgao ziada wa kiisimu wa mahusiano kati ya kitu na ulimwengu. Jedwali lifuatalo laonyesha utofauti uliopo kati ya jukumu mahali na umbo la uhusika mahali.

**Jedwali 3.2: Tofauti kati ya Jukumu Mahali na Umbo la Uhusika Mahali**

| | **Vichwa teule vya habari** | **Jukumu la uhsika** | **Umbo la uhusika** ( Viwakilishi vya ngeli ya 16, 17 na 18 kimofolojia) | **Ufafanuzi wa umbo la uhusika** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura | Mahali ( Pwani) | Uhuru na Ruto warudi Pwa-*ni* kutafuta kura | -*ni* |
| 2 | Viongozi wa ukambani wakutana na rais ikulu | Mahali (ukambani) | Viongozi wa Ukamba-*ni* wakutana na rais ikulu | -*ni* |
| 3 | Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini | Mahali (mazishini) | Raila aenda kuwakilisha nchi mazishi-*ni* | -*ni* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa | Mahali (Dubai) | Madiwani kustarehe *huko*, bajeti ikikashifiwa | *huko* (W. kionyeshi) |
| 5 | Viongozi wamtaka Jumwa ang'olewe uongozini | Mahali (Uongozini) | Viongozi wamtaka Jumwa ang'olewe uongozi-*ni* | -*ni* |

Jedwali 3.2 limeundwa kwa vichwa vya habari vitano, *Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura*, *Viongozi wa ukambani wakutana na rais ikulu*, *Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini*, *Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa* na *Viongozi wamtaka Jumwa ang'olewe uongozini*, ambavyo vimetumika kuonyesha utofauti uliopo baina ya jukumu mahali na umbo la uhusika mahali.

Katika uhusika mahali kiambishi *ni* kina majukumu mawili. Jukumu la kwanza ni kuwa, kiambishi hiki hutumika kama kijalizo katika neno na pili, hutumika kama kiwakilishi cha ngeli ya kumi na nane kimofolojia. Kulingana na Campe (1994), vijalizo ni mojawapo ya kategoria za kisintaksia ambazo hubainisha jukumu la uhusika katika sentensi. TUKI (2004) wanasema kuwa, kijalizo ni kipashio kikamilishacho kipashio kingine katika tungo au sentensi. Kiambishi tamati -*ni* kama kijalizo chajitokeza katika nomino zifuatazo: *Pwa-ni*, *ukamba-ni*, *mazishi-ni* na *uongozi-ni* kwenye vichwa vya habari, *Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura*, *Viongozi wa Ukambani wakutana na rais ikulu*, *Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini* na *Viongozi wamtaka Jumwa ang'olewe uongozini*, ili kuashiria undani wa sehemu au mahali fulani kitendo kilifanyika. Maana ibebwayo na

undani wa sehemu hizi, ndio jukumu mahali. Kichwa cha habari, *Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa*, hakina kijalizo *–ni* ambacho kinaweza kumwongoza mtafiti kubainisha jukumu lake, hivyo basi, mbinu ya kipimo cha kisemantiki imemwongoza mtafiti kubaini jukumu lengwa. Kwa mujibu wa Fillmore (1968), mbinu hii huhusisha mgao ziada wa kiisimu wa mahusiano kati ya kitendo na ulimwengu. Kitendo hapa ni; kustarehe kwa madiwani ughaibuni (Dubai) ilhali ulimwengu ni malalamiko ya wananchi kuhusu pesa wanazozitumia katika starehe zao bila kujali matakwa ya mwananchi wa kawaida. Kutokana na mahusiano haya na aina ya uhusika, neno la kimsingi ni *Dubai* na ndilo linaloashiria uwepo wa jukumu mahali katika kichwa lengwa cha habari.

Kwa kuwarejelea Samson na Schadeberg (1994) wakimnukuu Meinhof (1942), kiambishi tamati *-ni* kinaweza kutumika kama kiwakilishi kionyeshi cha ngeli ya 16, 17 na 18 kimofolojia. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa, maumbo ya uhusika katika vichwa vya habari, *Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura*, *Viongozi wa ukambani wakutana na rais ikulu*, *Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini*, *Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa* na *Viongozi wamtaka Jumwa ang'olewe uongozini*, ni viambishi tamati *–ni* vilivyoko katika virai nomino vifuatavyo vya ngeli ya 16, 17 na 18 kimofolojia; Pwa-*ni*, ukamba-*ni*, mazishi-*ni* na uongozi-*ni* mtawalia. Kando na kiambishi tamati *–ni*, viwakilishi vingine vinavyoweza kuchukua nafasi ya nomino za ngeli ya 16, 17 na 18 kimofolojia ni pamoja na, *hapa*, *humu*, *huku*, *huko*, *humo*, *kule*, *pale*, *hapo*, *mle* na kadhalika. Hivi ni viwakilishi vionyeshi vya mahali tendo lilitendekea.

Kiwakilishi kimoja kati ya hivi, huchukua nafasi ya kirai nomino, *Dubai*, katika kichwa cha habari, *Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa*, na kuwa umbo la uhusika. Kwa kuzingatia kigezo cha kisarufi, kiwakilishi *huko* ni faafu kutumika kwa niaba ya kirai nomino *Dubai*. Hivyo basi, umbo la uhusika katika kichwa cha habari teule ni kiwakilishi kionyeshi *huko*.

### 3.1.3 Tofauti kati ya Jukumu Ala na Umbo la Uhusika Ala

Kwa mujibu wa Blake (2004), jukumu ala huashiria chombo ambacho hutumika kutenda tendo. Mahusiano kati ya kiima na kiarifu katika sentensi hubainisha kifaa kilichotumika kutendea tendo hilo. Kifaa hicho ni jukumu ala. Ala si mojawapo ya nomino za kundi la 1/2 kimofolojia, hivyo basi, aina nyingine ya viwakilishi isipokuwa vya nafsi ina nafasi ya kuwa umbo la uhusika. Uteuzi wa kiwakilishi faafu kuchukua nafasi ya kirai nomino chenye uhusika ala ni lazima utilie maanani usahihi wa sentensi kimuundo na kisarufi. Jedwali 3.3 limetumika kama kielelezo.

**Jedwali 3.3: Tofauti kati ya Jukumu Ala na Umbo la Uhusika Ala**

| | **Vichwa teule vya habari** | **Jukumu la uhusika** | **Umbo la uhusika** (Kiwakilishi faafu huchukua nafasi ya kirai nomino lengwa) | **Ufafanuzi wa umbo la uhusika** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwanafunzi aliuawa kwa risasi – ripoti | Ala (risasi) | Mwanafunzi aliuawa *kwalo* – ripoti | *Kwalo* (W. kionyeshi) |
| 2 | 5 wahofiwa kufa ajali ya helikopta | Ala (helikopta) | 5 wahofiwa kufa kwa ajali *yayo* | *Yayo* (W. kionyeshi) |
| 3 | NASA waache mizaha ya kutumia Bibilia kujiapisha | Ala (Bibilia) | NASA waache mizaha ya kutumia *hiyo* kujiapisha | *hiyo* (W. kionyeshi) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Shoka la Obado latia hofu maafisa wakuu | Ala (shoka) | *Lake* latia hofu maafisa wakuu | *Lake* (W. kimilikishi) |
| 5 | Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi | Ala (Blockchain) | Teknolojia *yayo* itumiwe kuzima ufisadi | *Yayo* (W. kionyeshi) |

Vichwa vya habari vifuatavyo; *Mwanafunzi aliuawa kwa risasi – ripoti, 5 wahofiwa kufa ajali ya helikopta*, *NASA waache mizaha ya kutumia Bibilia kujiapisha*, *Shoka la Obado latia hofu maafisa wakuu na Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi,* katika Jedwali la 3.3 vimetumiwa kuonyesha tofauti iliyopo kati ya jukumu ala na umbo la uhusika ala.

Jukumu ala hutokana na mahusiano ya moja kwa moja kati ya kiima na kitenzi kikuu. Ala kama vile: risasi, helikopta, Bibilia, shoka na teknolojia ya blockchain vina nafasi ya kiarifu cha moja kwa moja katika muundo wa vichwa vya habari teule. Kinyume na kiima, kiarifu cha moja kwa moja si lazima kiwepo katika dhima ya kiisimu katika lugha. Kiarifu hiki hutokea tu pahali palipo na vitenzi elekezi kwani kinaweza kueleweka kwa upesi kando na kuonyeshwa wazi kila mara. Umbo la uhusika katika kichwa cha habari, *Mwanafunzi aliuawa kwa risasi – ripoti*, ni kiwakilishi kionyeshi, *kwalo* ilhali kiwakilishi kionyeshi, *yayo* ni umbo la uhusika katika vichwa vya habari, *5 wahofiwa kufa ajali ya helikopta* na *Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi*. Kichwa cha habari, *NASA waache mizaha ya kutumia Bibilia kujiapisha* kina kiwakilishi kionyeshi, *hiyo*

kama umbo la uhusika huku kiwakilishi kimilikishi (*lake*) kikiwa umbo la uhusika katika kichwa cha habari, *Shoka la Obado latia hofu maafisa wakuu*.

Kinyume na uhusika kiima ambao una viwakilishi nafsi kama maumbo ya uhusika pekee, uhusika ala huhusisha aina mbalimbali za viwakilishi kama maumbo ya uhusika. Katika Jedwali la 3.3, viwakilishi vionyeshi; *kwalo*, *yayo*, *hiyo* na kiwakilishi kimilikishi (*lake*) vimetumika kuashiria umbo la uhusika ala. Ukosefu wa viwakilishi nafsi kama umbo la uhusika katika aina hii ya uhusika ni kuwa, virai nomino vilivyo na uhusika ala si vya kundi la 1/2 kimofolojia, hivyo basi, nafasi yake haiwezi ikasimamiwa na viwakilishi nafsi.

### 3.1.4 Tofauti kati ya Jukumu Mtendwa na Umbo la Uhusika Yambwa

Gruber (1965) na Fillmore (1968) wanasema kuwa jukumu mtendwa huashiria hisia za tendo. Uhusiano uliopo hapa ni wa moja kwa moja kati ya mtendi, pigo na mtendwa. Kutokana na mahusiano haya, suala la mfuatano wa maneno katika sentensi hutumika ndipo kubainisha tofauti kati ya jukumu mtendi na jukumu mtendwa. Suala hili la mfuatano wa maneno katika sentensi hutambulika kama taipolojia ya kisintaksia ya lugha. Kittila, Vista na Ylikoski (2011) wanasema kuwa, mfuatano wa maneno katika sentensi iliyo na uhusika yambwa ni kama ifuatavyo: iwapo sentensi ipo katika hali ya kauli tendi, kiima hutanguliza huku kitenzi kikuu kikifuata na baadaye mpokezi wa pigo. Iwapo sentensi ipo katika hali ya kauli tendwa, mpokezi wa pigo huitanguliza kisha hufuatwa na pigo lenyewe na baadaye mtendi wa tendo. Hoja hii ndiyo itakayomwongoza mtafiti katika suala zima la kubainisha jukumu la mtendwa kutoka kwa uhusika yambwa.

Aghalabu, maumbo ya uhusika yambwa hutawaliwa na viwakilishi nafsi vya pili na tatu umoja na wingi. Viwakilishi nafsi huru hivi huwekwa katika nomino ambazo huhusishwa na kundi la binadamu pekee. Katika virai nomino ambavyo havihusishwi na kundi la binadamu, viwakilishi faafu kisintaksia huchukua nafasi ya virai nomino hivyo na kuwa umbo la uhusika kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la 3.4. Kwa mujibu wa Campe (1994), maumbo haya kimsingi huwa hayana maana bali huwakilisha msamiati tu. Jedwali lifuatalo limeweka wazi tofauti kati ya jukumu mtendwa na umbo yambwa.

**Jedwali 3.4: Tofauti kati ya Jukumu Mtendwa na Umbo la Uhusika Yambwa**

| | **Vichwa teule vya habari** | **Jukumu la uhusika** | **Umbo la uhusika** (Viwakilishi teule na faafu huchukua nafasi ya kirai-nomino) | **Ufafanuzi wa umbo la uhusika** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Sitaunga mtu yeyote kwa urais, gavana Ruto asema | Mtendwa (mtu yeyote) | Sitaunga *yeyote* kwa urais, Ruto asema | *Yeyote* (W. cha pekee) |
| 2 | Akashifu UhuRuto kwa mauaji | Mtendwa (UhuRuto) | Akashifu *wao* kwa mauji | *Wao* ni ( $W.nf._{2w}$) |
| 3 | Ahadi kuu ya Rais iwe ni kuliunganisha taifa | Mtendwa (taifa) | Ahadi kuu ya Rais iwe ni kuliunganisha *hili* | *Hili* (W. kionyeshi) |
| 4 | Ruto atetewa kuhusu 2022 | Mtendwa ( Ruto) | *Yeye* atetewa kuhusu 2022 | *Yeye* ni ( $W.nf._{3u}$) |
| 5 | Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani | Mtendwa (mwanawe Too) | Chama cha Jubilee chamteua *yeye* kuwa diwani | *Yeye* ni ( $W.nf._{3u}$) |

*Sitaunga mtu yeyote kwa urais gavana*, *Ruto asema*, *Akashifu UhuRuto kwa mauaji*, *Ahadi kuu ya Rais iwe ni kuliunganisha taifa*, *Ruto atetewa kuhusu 2022*, na *Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani*, ni baadhi ya vichwa

vya habari teule vilivyohusishwa katika Jedwali la 3.4 ndipo kubainisha tofauti iliyopo kati ya jukumu mtendwa na umbo la uhusika yambwa.

Katika Jedwali hili la 3.4, vichwa vya habari vifuatavyo viko katika hali ya kauli tendi; *Sitaunga mtu yeyote kwa urais gavana Ruto asema*, *Akashifu UhuRuto kwa mauaji*, *Ahadi kuu ya Rais iwe ni kuliunganisha taifa* na *Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani*. Jukumu la uhusika katika vichwa hivi vya habari lipo katika kirai nomino ambacho hufuata kitenzi kikuu. Kirai nomino: *mtu yeyote*, *UhuRuto*, *taifa* na *mwanawe Too* zina jukumu mtendwa. Hizi ndizo nomino zinazopokea pigo la mtendi moja kwa moja. Kiwakilishi nafsi cha tatu umoja (*yeye*) katika vichwa vya habari, *Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani* na *Ruto atetewa kuhusu 2022*, ndicho umbo la uhusika ilhali katika kichwa cha habari, *Akashifu UhuRuto kwa mauaji*, kiwakilishi nafsi cha pili wingi (*wao*) ni umbo la uhusika. Katika kichwa cha habari, *Ahadi kuu ya Rais iwe ni kuliunganisha taifa*, mahusiano ya moja kwa moja kati ya kitenzi *kuliunganisha* na nomino *taifa*, yanaibua uwepo wa kiwakilishi kionyeshi cha kirai nomino *taifa* ambacho ni *hili*. Hivyo basi, kiwakilishi kionyeshi (*hili*) ni umbo la uhusika la kichwa cha habari, *Ahadi kuu ya Rais iwe ni kuliunganisha taifa*. Umbo la uhusika katika kichwa cha habari, *Sitaunga mtu yeyote kwa urais gavana Ruto asema*, ni *yeyote*. Neno *yeyote* ni kiwakilishi cha pekee ambacho bado kipo katika kundi la viumbe hai. Jedwali la 3.4 lathibitisha maoni ya Krifka (1995) kuwa, aghalabu, viwakilishi vya kundi la binadamu hutawala maumbo ya uhusika yambwa kama ilivyojitokeza katika jedwali lengwa.

### 3.1.5 Tofauti kati ya Jukumu Tendea na Umbo la Uhusika Tendea

Kwa mujibu wa Fillmore (1968), jukumu tendea huashiria mwathiriwa wa tendo fulani. Jukumu hili hubainishwa kwa mahusiano ya moja kwa moja kati ya kitenzi na mwathiriwa wa tendo. Kitenzi kibebacho athari ya kirai nomino lengwa ndicho humwongoza mtafiti kubainisha jukumu la uhusika kwa matumizi ya kipimo cha kisemantiki. Ambapo, kitenzi hicho huoanishwa na ulimwengu ndipo kubainisha jukumu la kirai nomino lengwa. Sentensi yoyote iliyo na uhusika tendea huwa sahihi kisarufi na kimaana iwapo muundo wake unaashiria kiarifu kisichokuwa cha moja kwa moja cha kitenzi lengwa. Jedwali lifuatalo limeweka wazi tofauti iliyopo baina ya jukumu tendea na umbo la uhusika tendea.

**Jedwali 3.5: Tofauti kati ya Jukumu Tendea na Umbo la Uhusika Tendea**

| | **Vichwa teule vya habari** | **Jukumu la uhusika** | **Umbo la uhusika** (Viwakilishi nafsi huchukua nafasi ya kirai nomino) | **Ufafanuzi wa umbo la uhusika** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wezi waburudika kabla *kuibia* mwanasiasa | Tendea (mwanasiasa) | Wezi waburudika kabla kuibia *yeye* | *Yeye* ni ( W.nf.$_{3u}$) |
| 2 | Uamuzi wa KANU *kutoteua* mwaniaji wakanganya na kuwa mgawanyiko | Tendea (mwaniaji) | Uamuzi wa KANU kutoteua *yeye* wakanganya na kuwa mgawanyiko | *Yeye* ni ( W.nf.$_{3u}$) |
| 3 | UhuRuto wamefanya nifilisike, *afichua* Joho | Tendea (Joho) | UhuRuto wamefanya nifilisike, afichua *yeye* | *Yeye* ni ( W.nf.$_{3u}$) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Si ustaarabu walimu wapya *kutimuliwa* na wanasiasa | Tendea (walimu wapya) | Si ustaarabu *wao* kutimuliwa na wanasiasa | *Wao* ni ( W.nf.$_{3w}$) |
| 5 | Uhuru alite*ua* Nyachae kama njia ya kumzawadi | Tendea (Nyachae) | Uhuru aliteua *yeye* kama njia ya kumzawadi | *Yeye* ni ( W.nf.$_{3u}$) |

Katika Jedwali la 3.5, vichwa vya habari vifuatavyo; *Wezi waburudika kabla kuibia mwanasiasa*, *Uamuzi wa KANU kutoteua mwaniaji wakanganya na kuwa mgawanyiko*, *UhuRuto wamefanya nifilisike*, *afichua Joho*, *Si ustaarabu wanasiasa kutimua walimu wapya* na *Uhuru aliteua Nyachae kama njia ya kumzawadi*, vimetumiwa kama kielelezo cha kuashiria tofauti kati ya jukumu tendea na umbo la uhusika tendea.

Nomino *mwanasiasa*, *mwaniaji*, *Joho*, *walimu wapya* na *Nyachae* zimebeba jukumu tendea. Jukumu hili limetambulishwa kupitia mahusiano ya moja kwa moja kati ya vitenzi vyenye athari kwa virai nomino lengwa. Vitenzi hivi ni pamoja na; *kuibia*, *kutoteua*, *afichua*, *kutimuliwa* na *aliteua* mtawalia. Kwa matumizi ya kipimo cha kisemantiki, mahusiano kati ya vitenzi hivi na ulimwengu huibua jukumu tendea. Kitenzi, *kuibia* kina athari ya wizi kwa mwanasiasa ilhali kitenzi, *kutoteua* kina athari ya mgawanyiko wa chama cha KANU. Kitenzi, *fichua* kimebeba athari ya ufilisi kwa mwanasiasa Joho huku, tendo la *kutimuliwa* likiwaathiri walimu wapya. Athari ya kitenzi, *aliteua* laelekezwa kwa Nyachae. Athari hii ni ishara ya tuzo kwa Nyachae kutoka kwa rais Uhuru. Kutokana na

maelezo haya ni wazi kuwa, athari itokanayo na mahusiano kati ya nomino lengwa na kitenzi ni jukumu tendea la vichwa vya habari za siasa teule.

Viwakilishi vya nafsi ya pili wingi (*wao*) na tatu umoja (*yeye*) vimejitokeza kwa virai nomino vya ngeli ya 1/2 kimofolojia ili kuwakilisha umbo la uhusika katika vichwa vya habari teule kama ilivyoashiriwa katika Jedwali la 3.5.

### 3.1.6 Tofauti kati ya Jukumu Tokeo na Umbo la Uhusika Tokeo

Kwa mujibu wa Palmer (1994), jukumu tokeo huashiria zao la mwisho la kitendo. Kittila, Vista na Ylikoski (2011) wanasema kuwa, ndipo jukumu tokeo libainishwe, panafaa kuwa na sifa ya mwelekeo katika kitendo. Bora kuna dhana ya mwelekeo, iwe mwendo ulio na kikomo au mwendo usio na kikomo basi jukumu tokeo hubainika. Mahusiano kati ya mwelekeo huo na kinachosababisha mwelekeo wenyewe ndiyo jukumu tokeo. Kwa mujibu wa Fillmore (1968), mahusiano haya hutokana na mgao ziada wa kiisimu kati ya kitu na ulimwengu. Kama ilivyo katika aina nyingine za uhusika, viwakilishi teule na faafu huchukua nafasi ya umbo la uhusika. Jedwali lifuatalo laashiria utofauti uliopo kati ya jukumu la uhusika tokeo na umbo la uhusika tokeo.

**Jedwali 3.6: Tofauti kati ya Jukumu Tokeo na Umbo la Uhusika Tokeo**

| | **Vichwa teule vya habari** | **Jukumu la uhusika** | **Umbo la uhusika** (Viwakilishi teule na faafu huchukua nafasi ya kirai - nomino) | **Ufafanuzi wa umbo la uhusika** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wapwani wabuni muungano wao | Tokeo (muungano) | Wapwani wabuni *huo* wao | *huo* (W. kionyeshi) |
| 2 | Mudavadi kuongoza kampeni za NASA | Tokeo (kampeni za NASA) | Mudavadi kuongoza *hizo* | *hizo* (W. kionyeshi) |
| 3 | Miguna ageuzwa kipenzi cha Raila | Tokeo (kipenzi cha Raila) | Miguna ageuzwa *chake* | *chake* (W. kimilikishi) |
| 4 | Misururu ya kashfa haimbanduki Keter | Tokeo (misururu ya kashfa) | *Hiyo* haimbanduki Keter | *hiyo* (W. kionyeshi) |
| 5 | Tangatanga yadai wakuu walileta fujo | Tokeo (fujo) | Tangatanga yadai wakuu walileta *hiyo* | *hiyo* (W. kionyeshi) |

Jedwali 3.6 limeundwa kwa vichwa teule vya habari vitano, navyo ni; *Wapwani wabuni muungano wao*, *Mudavadi kuongoza kampeni za NASA*, *Miguna ageuzwa kipenzi cha Raila*, *Misururu ya kashfa haimbanduki Keter* na *Tangatanga yadai wakuu walileta fujo*. Vichwa hivi vimetumika kama kielelezo ili kuonyesha tofauti iliyopo kati ya jukumu tokeo na umbo la uhusika tokeo jinsi mtafiti anavyofafanua katika aya inayofuata.

Virai nomino *Muungano wao*, *kampeni za NASA*, *kipenzi cha Raila*, *misururu ya kashfa* na *fujo* ni viarifu vya moja kwa moja vitokanavyo na mahusiano kati ya

nomino *Wapwani*, *Mudavadi*, *Miguna*, *Keter*, *wakuu* na vitenzi *wabuni*, *kuongoza*, *haimbanduki*, *ageuzwa* na *walileta* mtawalia. Mahusiano haya yote yana sifa ya mwelekeo kama walivyoeleza Kittila, Vista na Ylikoski (2011). Kwa mfano; Kichwa cha habari, *Wapwani wabuni muungano wao* chaashiria kuwa, wapwani walikuwa wanachama wa miungano mingine ya kisiasa ambayo asili yake si pwani. Baada ya muda, wapwani wamefunguka macho na kuunda vuguvugu lao la kisiasa. Vuguvugu hili ndilo jukumu la uhusika tokeo. Sifa ya mwelekeo inajitokeza katika mwanzo wa mchakato wa uundaji wa muungano wa kisiasa wa pwani hadi hatua ya mwisho ya upatikanaji wa muungano huo. Kwa kuzingatia kichwa cha habari, *Tangatanga yadai wakuu walileta fujo*, ni wazi kuwa, eneo walilokuwa wanasiasa wa mrengo wa Tangatanga lilikuwa na amani kabla ya wakubwa kulivuruga. Sifa ya mwelekeo inajitokeza wazi kutoka kwa hali tuli hadi hali ya fujo. Zao la mwisho ambalo ni fujo ndilo jukumu la uhusika tokeo. Umbo la uhusika katika vichwa vya habari, *Wapwani wabuni muungano wao*, *Misururu ya kashfa haimbanduki Keter*, *Mudavadi aongoza kampeni za NASA* na *Tangatanga yadai wakuu walileta fujo*, ni viwakilishi vionyeshi, *huo*, *hiyo*, *hizo* na *hiyo* mtawalia. Katika kichwa cha habari, *Miguna ageuzwa kipenzi cha Raila*, kiwakilishi kimilikishi (*chake*) ndicho umbo la uhusika. Uhusika tokeo una aina tofauti za viwakilishi kama maumbo ya uhusika. Hii ni kwa sababu, virai nomino ambavyo hutiwa umbo la uhusika ni vya makundi mbalimbali ya ngeli, hivyo basi, viwakilishi hivyo vyafaa kuwa na uwiano wa kisarufi na sentensi lengwa.

Kwa kuzingatia zao la mwisho la sifa ya mwelekeo, jukumu tokeo hutambulishwa kwa upesi ilhali viwakilishi teule na faafu huwa maumbo ya uhusika tokeo kwa virai nomino lengwa katika sentensi.

## 3.2 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia tofauti iliyopo kati ya majukumu na maumbo ya uhusika. Viwakilishi nafsi vya nafsi ya pili na ya tatu vimetawala suala la maumbo ya uhusika. Kama ilivyoelezwa katika sura hii, Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu hazina mfumo wazi wa kiuhusika. Hivyo basi, hakuna maneno maalum yenye maana ambayo huweza kuchukua nafasi ya maumbo ya uhusika. Viwakilishi kwa ujumla huchukua nafasi ya maumbo ya uhusika katika aina mbalimbali za uhusika kama tu msamiati. Maumbo ya Kiswahili hayafungamanishwi na maana yoyote ila kuwa msamiati. Maumbo haya ni bia katika aina zote za uhusika. Viwakilishi nafsi ambata katika vitenzi huweza kubainisha ni aina gani ya umbo la uhusika yafaa kutiwa kwa virai nomino vilivyo na nomino za ngeli ya 1/2 kimofolojia.

Suala la majukumu ya uhusika ni dhahania. Jukumu la uhusika hubadilika kutoka aina moja ya uhusika hadi nyingine. Uhusika kiima una jukumu mtendi ilhali uhusika yambwa una jukumu mtendwa. Uhusika tendea, ala, mahali na tokeo zina majukumu tendea, ala, mahali na tokeo mtawalia. Katika kubainisha majukumu ya uhusika, viambajengo vya kisintaksia kama vile kiarifu cha moja kwa moja, kiarifu kisichokuwa cha moja kwa moja na kijalizo vimetumika ipasavyo.

# SURA YA NNE

# UMUHIMU WA SARUFI UHUSIKA KATIKA TAALUMA YA ISIMU

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu imebainisha dhahiri tofauti iliyopo kati ya majukumu ya uhusika na maumbo ya uhusika kwenye muundo wa sentensi. Hii ni sura iliyoonyesha wazi jinsi viwakilishi huchukua nafasi ya maumbo ya uhusika katika sentensi huku majukumu ya uhusika yakitokana na maana iibuliwayo na mahusiano ya maneno katika sentensi husika. Sarufi uhusika ina umuhimu anuwai katika taaluma ya isimu kama ilivyoangaziwa katika sura hii. Umuhimu huu umetokana na maoni yaliyoko katika utafiti wa sura ya kwanza hadi ya tatu.

## 4.1 Umuhimu wa Sarufi Uhusika katika Taaluma ya Isimu

Sarufi uhusika ina umuhimu anuwai katika taaluma ya isimu. Baadhi ya umuhimu huo ni; kurahisisha uelewaji wa sentensi katika lugha, kutambua kanuni za uundaji sentensi, kubainisha ubia wa maumbo ya uhusika, kuonyesha ubia wa ishara za uhusika katika lugha, kutambua dhima ya maneno katika tungo.

### 4.1.1 Kurahisisha Uelewaji wa Sentensi katika Lugha

Kwa mujibu wa Fillmore (1968), mfumo wa modeli ya uhusika huonyesha mahusiano ya ndani ya sentensi. Mahusiano haya huibuliwa na hali ya utangamano baina ya nomino au kiwakilishi chake na kitenzi kikuu. Kuhusiana huku kwa aina za maneno huibua maana kisemantiki ibebwayo na sentensi. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa, msomi wa isimu huongozwa na kigezo

cha mahusiano ya nomino au kiwakilishi chake na kitenzi kikuu ndipo kudondoa maana kisemantiki ya sentensi husika. Pia, kigezo hiki cha mahusiano ya maneno humpunguzia msomi fikira anuwai za jinsi ya kuifasiri kazi aliyoisoma kwani tayari huwa ana kielelezo cha kuzingatia. Maana bia kisemantiki huibuliwa kwa wasomi wote na ujumbe husika hueleweka ipasavyo bila ya nyongeza wala upungufu wa kimaana.

### 4.1.2 Kutambua Dhima ya Maneno katika Tungo

Sarufi uhusika imebainisha dhima ya maneno kama vile; virai nomino, vitenzi, viwakilishi na vihusishi katika sentensi. Uundaji wa sentensi yoyote ya Kiswahili ambayo ni sahihi kisintaksia huhusisha aina fulani ya uhusika. Uhusika huo hupatikana kwa kirai nomino kilichopo. Nomino ibebwayo na kirai nomino hicho huwa na dhima ya uhusika fulani. Dhima ya vitenzi na vihusishi katika sentensi ni sawia. Vyote ni vitambuzi vya uhusika. Mahusiano ya moja kwa moja baina ya kitenzi na nomino hutambua dhana ya uhusika katika sentensi lengwa. Vihusishi navyo hutiwa kabla ya kirai nomino lengwa ambacho hubeba aina fulani ya uhusika (Anderson 2006). Viwakilishi navyo ni maumbo ya uhusika katika tungo. Kwa mujibu wa Blake, (2004), maumbo haya huwa hayabebi maana yoyote ila huwa msamiati wa kiisimu tu. Sifa ya utoshelevu wa kiuteuzi, imemsaidia mtafiti kuangazia kila neno kama kiunzi, kisha kutambua dhima yake katika sentensi. Utambuzi wa dhima ya maneno katika sentensi ni mkabala rahisi ambao msomi wa kazi ya isimu anafaa kutumia wakati wa kudondoa maana kutoka kwa tungo fulani. Mkabala huu, huleta maana sawia baina ya wanaisimu mbalimbali, hivyo basi, suala la utata wa kimaana hufutiliwa mbali katika taaluma ya isimu.

Kulingana na Fillmore (1968), kila neno ambalo ni prediketa huwa na hoja. Si lazima neno ambalo ni prediketa liwe kitenzi pekee bali maneno toshelezi yaweza kuchukuliwa kama prediketa. Utambuzi wa maneno haya; nomino, vitenzi au viwakilishi unaweza kubainishwa na utendakazi wa kanuni za lugha husika. Maneno mengi toshelezi yanaweza kutumika kama prediketa ila lugha nyingi zina sheria ambazo hugeuza kitenzi kikuu kuwa kitenzi kishirikishi huku nomino na kiwakilishi zikichukua nafasi ya prediketa. Hata hivyo, baadhi ya lugha hukubali prediketa ya kawaida. Pia, viunganishi kama vile; *kwa sababu* vinaweza kuchukuliwa kama prediketa kwani vinaweza vikaelezwa kulingana na idadi ya hoja zinazobeba.

### 4.1.3 Usarufi wa Tungo

Kulingana na Habwe na Karanja (2004), tungo huwa sahihi kisarufi iwapo maungano na mahusiano ya maneno ni sahihi na yenye maana. Umuhimu mwingine wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu ya Kiswahili ni utambuzi wa usahihi wa sentensi kisarufi. Hackmack (2015), akimnukuu Meinhof (1906) anasema kuwa, mahusiano ya maneno katika sentensi yanahusishwa na utendakazi wa kiisimu wa kiima, kiarifu cha moja kwa moja, kiarifu kisichokuwa cha moja kwa moja, vijalizo na kadhalika. Katika isimu, uhusika ni maumbo ambayo nomino au viwakilishi huchukua ndiposa kueleza mahusiano yaliyopo katika sentensi. Kwa mfano; muundo wa uhusika kiima huwa sahihi kisarufi iwapo kiima huashiriwa kama kielezo bayana cha kitenzi chenye kukubaliana na nomino katika idadi na nafsi.

a. Mama anapika ugali (sahihi kisarufi)

Uhusika kiima (mama) unakubaliana na kitenzi pika na nomino ugali katika idadi na nafsi.

b. Baiskeli wanalima shamba (si sahihi kisarufi)

Uhusika kiima (baiskeli) haukubaliani na kitenzi lima na nomino shamba katika idadi na nafsi. Binadamu au pengine ng'ombe ndio walio na uwezo wa kulima shamba. Sentensi hii ni potovu kisarufi na kimaana.

Sentensi yoyote iliyo na uhusika tendea huwa sahihi kisarufi na kimaana iwapo muundo wake unaashiria kiarifu kisichokuwa cha moja kwa moja cha kitenzi lengwa. Kwa mfano; *Wezi waburudika kabla kuibia mwanasiasa*, ni tungo sahihi kisarufi na kimaana. Miundo ya sentensi yenye uhusika yambwa na ambayo ni sahihi kisarufi huashiriwa na kiarifu cha moja kwa moja cha kitenzi. Kwa mfano; Mama alimpiga mtoto. Katika uhusika ala, usarufi wa tungo hujitokeza pale ambapo uhusika ala hutokea kama kiima cha kitenzi au kiarifu cha moja kwa moja cha kitenzi. Kwa mfano; *Kisu kilitumika kumchinja mbuzi* (kiima cha kitenzi – sahihi kisarufi na kimaana), *Alimkata kwa kisu* (kiarifu cha moja kwa moja - sahihi kisarufi na kimaana). Kiambishi tamati *–ni* ambacho huongezewa kwenye nomino zinazoashiria eneo fulani ndipo kuonyesha mahali ambapo tendo lilitendeka huleta usarufi wa tungo katika sentensi zenye uhusika mahali. Kwa mfano; Bosco alienda shamba*ni*. Usarufi wa tungo katika sentensi zilizo na muundo wa uhusika tokeo hubainika baada ya kiarifu kuathirika. Kwa mfano;

*Wapwani wabuni muungano wao*. Kwa kuzingatia usarufi huu, mtu yeyote anaweza akazalisha sentensi anuwai za isimu ya Kiswahili, hivyo kuikuza isimu ya Kiswahili.

### 4.1.4 Kukua kwa Matumizi ya Istilahi za Isimu ya Kiswahili ambazo Msingi wake ni Sarufi Zalishi

Msingi wa baadhi ya istilahi za isimu zilizotumika katika utafiti huu umetokana na kazi za awali za Noam Chomsky. Handoko (2010) anasema kuwa, mnamo mwaka wa 1957 Chomsky alipendekeza muundo wa kisintaksia uliotoa maelezo kuwa, ingekuwa bora zaidi iwapo sarufi ya lugha ingeangaziwa kama mfumo unaojitawala na usiotegemea mifumo mingine ya lugha kama vile; semantiki na fonolojia. Maoni haya yalimchochea Chomsky kuasisi dhana ya sarufi zalishi geuzi mnamo mwaka wa 1965 katika kitabu chake cha; *Aspects of Theory of Syntax*. Katika kitabu hicho, Chomsky alibainisha kuwa, sentensi huwa na kategoria mbili kuu, nazo ni; muundo ndani na muundo nje. Pia, alitambua kuwa sentensi huundwa na miundo mbalimbali ya viambajengo. Miundo ya viambajengo hivi ni pamoja na; kategoria virai na kategoria leksia. Istilahi kama vile; kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kihusishi na kadhalika ni mojawapo ya viambajengo vya kategoria virai. Kategoria leksia ilihusisha istilahi za isimu zifuatazo; nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi, kiwakilishi, kihusishi, kiunganishi na kihisishi. Matumizi ya kategoria hizi mbili kuu za sentensi (*muundo ndani* na *muundo nje*) pamoja na istilahi za isimu alizoasisi Chomsky mnamo mwaka wa 1965 katika utafiti huu ni njia mojawapo ya kuzikuza na kuzipanua kimatumizi. Jinsi umbo la ndani la sentensi lilivyo la kimsingi katika kazi za Chomsky za

mwaka wa 1965, ndivyo umbo hilo lilivyo la kimsingi katika utambulishaji wa aina ya uhusika kwenye sentensi katika kazi za Fillmore, 1968. Muundo ndani wa sentensi una jukumu sawia katika kazi za Chomsky 1965 na Fillmore 1968. Jukumu lake ni kutoa maana ibebwayo na viambajengo vinavyounda sentensi lengwa.

Kwa mujibu wa Chomsky (1965), kanuni za sarufi miundo virai hutambulisha maumbo msingi ya sentensi. Kanuni hizi hutumia alama kama vile;

| | |
|---|---|
| S | Sentensi |
| N | Nomino |
| T | Kitenzi |
| V | Kivumishi |
| E | Kielezi |
| W | Kiwakilishi |
| U | Kiunganishi |
| HU | Kihusishi |
| HI | Kihisishi |

Alama hizi za aina ya maneno huweza kutumiwa kujenga virai ambavyo vinaweza kuwakilishwa katika alama zifuatazo;

| | |
|---|---|
| KN | Kirai nomino |
| KT | Kirai Kitenzi |
| KV | Kirai kivumishi |
| KE | Kirai kielezi |
| KH | Kirai kihusishi |

Nadharia ya uhusika ya Fillmore (1968), imekuza na kupanua matumizi ya sheria hizi katika isimu ya Kiswahili kupitia mchakato wa utiaji uhusika kwenye sentensi. Kwa mfano;

**4.1 Kielelezo cha utiaji uhusika tokeo**

a) Muundo nje



a

sema nia ni kuzuia mshindi katika raundi ya kwanza kwenye uchaguzi ujao

Wapwani wabuni muungano wao

20/2/2017

a) Muundo ndani




*S* → *KL+HL*

*KL* → *T+UH+UH*$_n$

*UH* → *K+KN*

Kanuni tatu kuu za utiaji uhusika zifuatazo; *S* $\rightarrow$ *KL+HL*, *KL* $\rightarrow$ *T+UH+*$UH_n$ na *UH* $\rightarrow$ *K+KN* zimeutambua muundo ndani wa kichwa cha habari, *Wapwani wabuni muungano wao*. Istilahi kama vile; sentensi na kirai nomino ambazo asili yake ni sarufi zalishi zimetumika.

Kanuni ya kwanza (*S* $\rightarrow$ *KL+HL*) ina maana kuwa, kichwa cha habari; *Wapwani wabuni muungano wao* kimegawa katika sehemu mbili kuu, nazo ni; kauli na hali kama ilivyoonyeshwa katika Kielelezo 4.1. Sehemu ya hali ina njeo pekee (wakati uliopo) ilhali sehemu ya kauli ina mgao ziada unaohusisha kitenzi na uhusika lengwa. Neno *buni* ndilo kitenzi katika sehemu ya kauli ilhali kirai nomino *muungano wao* kimebeba nomino iliyo na uhusika tokeo (*KL* $\rightarrow$ *T+*$UH_n$). Kanuni ya tatu (*UH* $\rightarrow$ *K+KN*) inatambulisha nomino iliyo na uhusika tokeo. Kanuni hii hutambua ishara za uhusika ambazo hutanguliza kirai nomino kibebacho nomino iliyo na uhusika lengwa. Katika Kielelezo 4.1, ishara ya uhusika kabla ya nomino iliyo na uhusika tokeo ni kapa ilhali nomino *muungano* ni uhusika tokeo. Matumizi ya sheria hizi katika vigezo mbalimbali vya sarufi kama vile, uhusika yanakuza isimu ya lugha ya Kiswahili.

Hackmack (2015) anasema kuwa, istilahi za hali, uhusika, idadi, njeo na utendakazi wa kiisimu kama vile; kiima na kiarifu zimetawala isimu ya Kiswahili. Maoni haya yanaungwa mkono na Amidu (2004) anayesema kuwa, waandishi walitumia istilahi zoefu katika isimu ya Kijerumani na Kilatini. Isimu hizi, hutambulika kufanya kazi chini ya mchakato wa tafsiri (isimu tafsiri) vivyo hivyo

ndivyo ilivyo Kiswahili. Isimu tafsiri imejengeka katika mhimili kuwa, mwanaisimu anapopata maarifa ya isimu ya Kijerumani, Kilatini au Kiingereza anachohitaji ndipo kuandika isimu ya Kiswahili ni, kuwasilisha mawazo yake kwa namna ambayo wananchi wa nchi zizungumzao Kijerumani, Kilatini au Kiingereza wanaweza kuelewa. Hivyo basi, isimu tafsiri ya Kiswahili huhusisha; tafsiri ya mawazo ya Kiswahili kuwa Kijerumani, Kilatini au Kiingereza, uchanganuzi wa tafsiri hiyo ya Kijerumani, Kilatini au Kiingereza yenye miundo ya maneno na sentensi na matumizi ya miundo hiyo katika vigezo mkabala katika data ya Kiswahili.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa, utafiti unaoambatana na istilahi za kiisimu kama vile; kirai nomino, kirai kitenzi, njeo, hali, kauli, kiarifu, kiima na uhusika ni nyongeza ya maarifa katika isimu ya Kiswahili. Maarifa haya yamekuza lugha ya Kiswahili.

## 4.2 Hitimisho

Sura ya nne imeshughulikia umuhimu wa sarufi uhusika katika isimu. Umuhimu huu umetajwa na kufafanuliwa kwa upana kutokana na utafiti uliofanywa kwenye sura ya kwanza hadi ya tatu. Masuala muhimu yaliyoangaziwa katika sura hii ni; urahisishaji uelewaji wa sentensi katika lugha, utambuzi wa dhima ya maneno katika tungo, usarufi wa tungo na ukuzaji wa matumizi ya istilahi za isimu ya Kiswahili ambazo msingi wake ni sarufi zalishi. Umuhimu wa hoja hizi katika taaluma ya isimu ya Kiswahili umefafanuliwa kwa upana kwenye Sehemu ya 4.1

ya sura hii. Sura inayofuata hii ni ya tano. Sura hii ya tano ni ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii inahusisha hitimisho la utafiti jinsi inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura zilizotangulia, mtafiti amechunguza jinsi uhusika hujitokeza katika vichwa vya habari za siasa. Kinyume na sura hizo, sura hii nayo imehitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari wa sura ya kwanza, pili, tatu na nne. Pia, matokeo ya utafiti huu, mchango wake katika isimu ya Kiswahili, changamoto alizokumbana nazo mtafiti na mapendekezo ya tafiti za baadaye kwa ajili ya kukuza isimu ya Kiswahili yameelezwa.

### 5.1.1 Muhtasari wa Utafiti

Huu ni utafiti uliolenga kubainisha dhana ya uhusika katika magazeti ya *Taifa Leo*. Dhana hii ilidhamiriwa kubainishwa kwa kuzingatia malengo yafuatayo: kudhihirisha na kuchambua dhana mbalimbali za uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo*, kutofautisha majukumu ya uhusika na maumbo ya uhusika katika vichwa vya habari za siasa kwenye gazeti la *Taifa Leo* na kubainisha umuhimu wa sarufi uhusika katika taaluma ya isimu.

Sura ya kwanza ni muhtasari wa mwelekeo wa utafiti unaohusisha masuala yafuatayo: ufafanuzi wa istilahi muhimu, usuli wa mada, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia, mbinu za utafiti, uteuzi wa

sampuli, mbinu za ukusanyaji data, maadili ya utafiti, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

Katika sura ya pili, mtafiti amedhihirisha aina sita za uhusika na jinsi uhusika huo hujitokeza katika sentensi kwa mujibu wa Fillmore (1968). Hii ni sura iliyokusudia kuonyesha kategoria mbili za sentensi: muundo ndani na muundo nje na jinsi mahusiano ya maneno katika sentensi hizo huibua maana kisemantiki ya vichwa teule vya habari za siasa vilivyoko katika magazeti ya *Taifa Leo*.

Suala la umbo la uhusika na majukumu ya uhusika limeshughulikiwa katika sura ya tatu. Hii ni sura iliyokusudia kuonyesha tofauti iliyopo kati ya umbo la uhusika na jukumu la uhusika katika sentensi. Katika sura hii, mtafiti amebainisha kuwa majukumu ya uhusika ni anuwai ilhali maumbo yake ni bia. Jukumu la uhusika hutegemea aina ya uhusika lengwa ilhali nafasi ya umbo la uhusika huchukuliwa na viwakilishi.

Sura ya nne imetoa maelezo ya umuhimu wa dhana ya kisarufi ya uhusika kwa ukamilifu. Baadhi ya umuhimu huo ni; kurahisisha uelewaji wa sentensi katika lugha, matumizi ya ubia wa maumbo ya uhusika kisarufi, utambuzi wa kanuni za uundaji sentensi, utambuzi wa ishara za uhusika katika lugha, utambuzi wa dhima ya maneno katika tungo, ukuzaji wa matumizi ya istilahi za isimu ya Kiswahili na usarufi wa tungo. Huu ni umuhimu ambao umechangia maarifa ya ziada katika taaluma ya isimu.

Kwa ujumla, huu ni utafiti uliozingatia nadharia ya uhusika iliyoasisiwa na Fillmore (1968). Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ambapo, vichwa teule thelathini vya habari za siasa kutoka kwa magazeti anuwai ya *Taifa Leo* vilikusanywa kama data na kuchambuliwa. Ukusanyaji wa data hii ulitumia mbinu ya upekuzi wa yaliyomo huku usampulishaji kimakusudi uliongozwa na kigezo cha siasa ukitumika kuteua sampuli lengwa. Malengo ya utafiti huu yaliafikiwa ipasavyo huku data ikichanganuliwa vilivyo kwa michoroti ya kisintaksia na kuwasilishwa kwa majedwali yaliyoandamana na maelezo mafupi.

### 5.1.2 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na uchambuzi wa data teule iliyowasilishwa, matokeo yafuatayo yalibainishwa: aina mbalimbali za uhusika hupatikana katika miundo mbalimbali ya vichwa vya habari za kisiasa. Aina hizo za uhusika ni; uhusika kiima, ala, tendi, yambwa, tokeo na mahali. Uwepo wa aina hizi za uhusika katika vichwa vya habari za siasa unathibitisha maoni ya Fillmore (1968) kuwa, isimu ya Kiswahili ina aina sita za uhusika.

Kichwa chochote cha habari za siasa huwa na kategoria mbili za uwakilisho, nazo ni: muundo ndani na muundo nje. Muundo ndani ni dhahania ilhali muundo nje huonekana. Maana katika kichwa cha habari teule hudondolewa kwenye muundo ndani wa kichwa hicho. Muundo ndani wa kichwa cha habari teule hugawanishwa katika sehemu mbili kuu; kauli na hali. Sehemu ya hali huonyesha wakati kitendo kilitendeka ilhali sehemu ya kauli uhusisha kitenzi na mfuatano wa aina mbalimbali za uhusika zilizopo kwenye kichwa cha habari teule. Kabla ya utiaji

uhusika katika kichwa cha habari teule, ishara za uhusika faafu hutanguliza virai nomino vibebavyo nomino zilizo na uhusika lengwa. Ishara hizo za uhusika aghalabu huwa vihusishi na kiambishi tamati *–ni*. Pale ambapo kihusishi hakitangulizi kirai nomino kibebacho nomino yenye uhusika lengwa, ishara kapa (*Ø*) ya uhusika huchukua nafasi ya umbo la uhusika.

Katika sura ya tatu, mtafiti alibainisha tofauti iliyopo kati ya maumbo ya uhusika na majukumu ya uhusika. Michoro ya majedwali ilitumika ndipo kuonyesha mpaka uliopo kati ya umbo na jukumu la uhusika. Utafiti huu ulionyesha kuwa, Kiswahili hakina maumbo dhahiri ya uhusika isipokuwa viwakilishi nafsi vya nafsi ya pili na tatu, umoja na wingi. Hivyo basi, miundo mingine ya sentensi ambayo huhitaji maumbo ya uhusika kando na umbo la viwakilishi nafsi, viwakilishi vya ngeli ya nomino lengwa huchukua nafasi hiyo. Aghalabu, maumbo ya uhusika katika vichwa vya habari teule za siasa zenye uhusika kiima, yambwa na tendea ni viwakilishi nafsi vya pili na tatu, umoja na wingi (*wewe*, *yeye*, *wao*, *nyinyi*) katika ngeli ya 1/2 kimofolojia. Mara nyingi, katika uhusika mahali, kiambishi tamati *-ni* ambacho ni kiwakilishi cha ngeli ya 18 kimofolijia huchukua nafasi ya umbo la uhusika. Pale ambapo kiambishi tamati *–ni* hukosekana katika nomino lengwa inayoashiria uhusika mahali, kiwakilishi kionyeshi faafu huchukua nafasi hiyo, kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la 3.2, ukurasa wa 60-61. Viwakilishi vionyeshi na viwakilishi vimilikishi faafu huchukua nafasi ya umbo la uhusika katika vichwa vya habari za siasa zenye uhusika ala. Hili limethibitishwa katika Jedwali la 3.3, ukurasa wa 63 na 64. Aina

nyingine ya viwakilishi isipokuwa viwakilishi vya ngeli ya 1/2 kimofolojia ni umbo la uhusika katika vichwa vya habari za siasa vilivyo na uhusika tokeo. Uteuzi faafu wa maumbo haya ya uhusika hutegemea upatanisho wa kisarufi kati ya nomino lengwa na maneno mengine yanayounda kichwa cha habari teule kama ilivyoonyeshwa katika jedwali 3.6, ukurasa wa 71. Jedwali hili linaashiria kuwa, viwakilishi vionyeshi na vimilikishi ni mojawapo ya maumbo ya uhusika tokeo katika vichwa vya habari za siasa zenye uhusika tokeo.

Utafiti huu umebainisha umuhimu mbalimbali wa dhana ya uhusika katika isimu. Kisarufi, msomi wa makala ya magazeti amebaini kuwa vichwa vya habari katika magazeti huwa na kategoria mbili za uwakilisho: muundo ndani na muundo nje. Ambapo, uwakilisho huu una sehemu mbili kuu: kauli na hali. Muundo wa nje huonekana ilhali muundo ndani ni dhahania na ndio hubeba maana ya kichwa teule cha habari. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa, kisintaksia, mgao wa vichwa teule vya habari katika vijisehemu humsaidia msomi wa kazi ya isimu kujua viambajengo vilivyoviunda. Baada ya kutambua viambajengo hivyo, kwa wepesi, mtafiti huweza kubaini maana ibuka kisemantiki itokanayo na mahusiano ya viambajengo hivyo. Ushirikiano baina ya kipengele cha kisintaksia na kisemantiki huibua maana isiyokuwa na utata wowote katika tungo lengwa. Istilahi za isimu ya Kiswahili zilizoasisiwa kipindi cha sarufi zalishi kama vile kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kihusishi na kadhalika zimekuzwa kimatumizi. Alama za uwakilisho kama vile KN (kirai nomino), KT (kirai kitenzi), KH (kirai kihusishi), N (nomino), T (kitenzi), E (kielezi) na kadhalika bado zinatumika

katika sarufi ya sasa. Matumizi ya ishara hizi za uwakilisho pamoja na istilahi zenyewe yamekuza na kupanua mno mawanda ya msamiati wa isimu ya Kiswahili.

### 5.1.3 Changamoto ya Utafiti

Utafiti huu umefanywa wakati ambao taifa la Kenya limekuwa na kipindi kigumu sana cha kupambana na virusi vya korona. Kutokana na sheria zilizowekwa na serikali ndipo kuzuia msambao wa gonjwa hili, vyuo vyote vya mafunzo vilifungwa kwa muda. Ufungaji wa vyuo hivi ulisababisha ongezeko la gharama ya utafiti na kipindi cha utafiti. Mtafiti hakuwa na budi ila kujisimamia gharama za mtandao wa mawasiliano ya kimataifa kwenye kompyuta kwa ajili ya kupakua makala na vitabu vilivyomsaidia katika utafiti wake. Wakati mwingine, mtandao huu haukufanya kazi ipasavyo kwa sababu ya ubovu wa wavu wake katika eneo la mashambani. Tukio hili lilimfanya mtafiti akawie katika utafiti wake hadi wakati ambapo wavu wa mtandao huo ungeimarika.

### 5.1.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mtafiti mwingine anaweza kulishughulikia suala lili hili kwa kuzingatia nadharia ii hii bali data yake ya uchambuzi iwe tofauti na ya kisiasa. Vichwa vya habari za michezo, lugha, afya, ugatuzi, maendeleo ya nchi, masuala ya nchi za kigeni na kadhalika vinaweza kutumika kama data ya utafiti. Pia, mtafiti huyo anafaa kutumia aina nyingine ya magazeti kando na gazeti la *Taifa Leo* lililotumika katika utafiti huu. Baadhi ya magazeti hayo ni; gazeti la *Pambazuko*, *Mwanaspoti* na kadhalika.

### 5.2 Hitimisho

Katika sura hii, muhtasari wa matokeo, changamoto za utafiti na mapendekezo umefanywa. Sehemu ya muhtasari imetoa maelezo ya jinsi utafiti huu ulivyofanywa pamoja na namna malengo ya utafiti yaliafikiwa. Matokeo ya utafiti huu yametokana na majibu ya maswali ya utafiti ambayo yameunda sura ya pili, tatu na nne. Mapendekezo nayo yametolewa ndiposa kudhihirisha pengo zilizopo katika sarufi uhusika na jinsi ambavyo zinaweza kufanyiwa utafiti zaidi kwa ajili ya kukuza isimu ya Kiswahili.

## Marejeleo

Amidu, A.A (2004). Kiswahili Language Description and Translational Grammar. *Journal of Linguistics 2.1, pp 45-58*. Retrieved from: *www.fb10. Unibremen.de/homepages/hackmack/morphologie/pdf/Texte-SH/ Case-Swahili.pdf*

Anderson, J.M (2006). *Modern Grammars of Case*. New York: Oxford University Press.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Press.

Barasa, L. & Kazungu, K. (2017). Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura. *Taifa Leo*, 14, 2017.

Bernstein, I. (1971). *An Introductory Transformational Grammar*. Eaglewood Cliffs: Prentice Hall Inc.

Bílý, M. (1990). The Case Remains Open (Some Notes on a New Book on Morphological Case in Russian) [Review of *Kasus. Zur Explikation eines sprachwissenschaftlichen Terminus (am Beispiel des Russischen)*, by H.-E. Seidel]. *Russian Linguistics*, *14*(2), 185–203. http://www.jstor.org/stable/ 40160274

Blake, B. J. (2004). *Case*: New York. Cambridge University Press.

Bocha, G. (2017). Wapwani wabuni muungano wao. *Taifa Leo*, 20, 2017.

Bretch, R.D & Levine, J.S (1986). *Case Meaning*. Columbus, Ohio: Slavica Press.

Bussmann, H. (1996). *Routledge Dictionary of Language and Linguistics*. London: Routledge Press.

Campe, P. (1994). *Case, Semantic roles and Grammatical relations*. Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Chafe, W. L. (1970). *Meaning and the Structure of Language*. Chicago: University of Chicago Press.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of Theory of Syntax*. Cambridge: Cambridge University Press.

Collins, H. (2012). *Collins English Dictionary*. Wellington. New Zealand Press.

Cook, V. J (1988). *Chomsky's Universal Grammar*. Oxford: Basil Blackwell Press.

Fillmore, C. J. (1968). *The Case for Case in Bach and Harms* (*Ed*.). *Universal in Linguistic Theory*. New York: Holt Rinehart and Winston Press.

Fillmore, C. J. (1987). *The case for case* (*Ed.*). *Universal in Linguistic Theory*. New York: Holt Rinehart and Winston Press.

Gruber, J.S. (1965). *Studies in Lexical Relations*. Published PhD Dissertation. MIT Press.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Press.

Hackmack, S. (2015). Case In Selected Grammars of Swahili. *Journal of Colonialism and Missionary Linguistics, pp 51-74.* Retrieved from:

*www.fb10.uni-bremen.de/homepages/hackmack/morphologie/pdf/Texte-SH/Case_Swahili.pdf*

Handoko, H. (2010). *Transfomational Generative Grammar Analysis of English Imperative as found in "Lie to me" season 1 TV series*. Unpublished M.A Thesis: Dharma Andalas University

Hatch, E. (1992). *Discourse and Language Education*. Cambridge: Cambridge University Press.

Janda, L. A. (1993). *A Geography of Case Semantics*: The Czech Dative and the Russian Instrumental. Berlin: Mouton Press.

Kamau, W. (2018). Ruto atetewa kuhusu 2022. *Taifa Leo*, 9, 2018.

Kamau, W. (2019). Raila amkemea Matiang'i. *Taifa Leo*, 10, 2019.

Kamau, W. (2018). Misururu ya kashfa haimbanduki Keter. *Taifa Leo*, 19, 2018.

Kamau, W. (2018). NASA waache mizaha ya kutumia bibilia kujiapisha. *Taifa Leo*, 24, 2018.

Kamau, W. (2018). Uhuru aliteua Nyachae kama njia ya kumzawadi. *Taifa Leo*, 25, 2018.

Karichia, J. K. (2012). *Usawiri wa Wanasiasa kama Wahusika katika Makala za Habari kwenye Gazeti la Taifa Leo Nchini Kenya*. Unpublished M.A. Thesis: Kenyatta University.

Kaviti, M. F. (2005). *Makosa ya Kisintaksia katika Tafsiri za Makala Magazetini*. Unpublished M.A Thesis: Kenyatta University.

Kilalo, L. & Ahmed, M. (2017). Viongozi wa Ukambani wakutana na Rais ikulu. *Taifa Leo*, 12, 2019.

Kimalu, P. K. & Marimba (2014). *Research Methods Monitoring and Evaluation*. Nairobi: Kamumi Enterprise Limited.

Kimei, T. (2017). Sitaunga mtu yeyote kwa urais, Gavana Ruto asema. *Taifa Leo*, 16, 2017.

King'ori, A. W. (2005). *Movement in the Kiswahili Sentence*: *A Minimalist Approach*. Unpublished M.A. Thesis: Kenyatta University.

Kittila, K., Vista, K. na Ylikoski, J. (2011). *Case, Animacy and Semantic Roles*: Amsterdan. John Benjamins Publishing Company.

Krifka, M. (1995). Swahili, in: Jacobs, Joachim et al. (eds): *Syntax. Ein internationales Handbuch zeitgenössischer Forschung. 2. Halbband [HSK 9,2] :* Berlin/New York. de Gruyter, Seiten.

Leech, G. N. & Short, M. H. (1981). *Style in Fiction*: *A Linguistic Introduction to English Fictional Prose.* New York: Longman Group Limited.

Lubanga, D. (2019). Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani. *Taifa Leo*, 9, 2019.

Luita, S. (2017). 5 wahofiwa kufa ajali ya helikopta. *Taifa Leo*, 21, 2017.

Lwanga, C. (2019). Viongozi wataka Jumwa ang'olewe uongozini. *Taifa Leo*, 10, 2019.

Magoma, E. M. (2015). *Fani na Maudhui katika Mashairi ya Magazetini*. Unpublished M.A. Thesis: Kenyatta University.

Marshall, C. & Rossman, B.G. (1995). *Designing Qualitative Research*. London: SAGE Press.

Matheka, B. (2018). Ahadi kuu ya Rais iwe kuliunganisha Taifa. *Taifa Leo*, 5, 2018.

Mann, W.C. & Thompson, S.A. (1987). *Rhetorical Structure Theory*. *A Theory of Text Organization*. California: University of South California Press.

Mugenda, A.G. (2013). *Qualitative Research Methods. Introduction*. Nairobi: ACTS Press.

Munene, G. (2017). Karua asukumwa kuondoa kesi yake dhidi ya Waiguru. *Taifa Leo*, 19, 2017.

Mvati, M., Maina, R., na Kanuri, J. (2004). *Miale ya Sarufi*. Nairobi: The Franciscan Kolbe Press.

Naswa, A. K. (2003). *The Syntax of Noun Phrase Movement in Kiswahili*. Unpublished M.A. Thesis: Kenyatta University.

Newmeyer, F. (2010). Comparative concepts and descriptive categories. A reply to Haspelmath, in: *Language 86.3, 688–695*.

Ngila, F. (2018). Teknolojia ya Blockchain itumiwe kumaliza ufisadi. *Taifa Leo*, 7, 2018.

Njeru, A. (2017). Uhuruto wamefanya nifilisike, afichua Joho. *Taifa Leo*, 22, 2017.

Njeru, A. (2018). Madiwani kustarehe Dubai, bajeti ikikashifiwa. *Taifa Leo*, 4, 2018.

Nyongesa, B.W. (2005). *Kenyan Newspaper Discourse: An Investigation of Rhetorical Structure in Editorials as Argumentation*. Unpublished M. A. Thesis: Kenyatta University.

Obara, V. (2017). Mudavadi kuongoza kampeni za NASA. *Taifa Leo*, 20, 2017.

Obara, V. & Kamau, W. (2018). Miguna ageuzwa kipenzi cha Raila. *Taifa Leo*, 8, 2018.

Obara, V. (2018). Si ustaarabu wanasiasa kutimua walimu wapya. *Taifa Leo*, 15, 2018.

Odhiambo, N. (2017). Akashifu UhuRuto kwa mauaji. *Taifa Leo*, 3, 2017.

Onyango, L. (2017). Uamuzi wa KANU kutoteua mwaniaji wakanganya. *Taifa Leo*, 2, 2017.

Oudia, R. & Oketch, A. (2017). Mwanafunzi aliuawa kwa risasi-Ripoti. *Taifa Leo*, 10, 2017.

Palmer, F. R. (1994). *Grammatical Roles & Relations*. New York: Cambridge University Press.

Samson, R. & Schadeberg, T.C (1994). Kiinimacho cha mahali, kiambishi tamati ni-. *Swahili Forum. AAP 37, pp 127-138*.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wainaina, E. (2017). Wezi waburudika kabla kuibia mwanasiasa. *Taifa Leo*, 3, 2017.

Wanyoro, C. & Ondieki, E. (2018). Sitangatangi, Ruto ajitetea. *Taifa Leo*, 3, 2018.

Wesonga, C. (2017). Musila ajiondoa Wiper baada ya kushindwa. *Taifa Leo*, 4, 2017.

Wesonga, C. (2018). Uhuru atema Mawaziri 13. *Taifa Leo*, 6, 2018.

Wesonga, C. (2019). Tangatanga yadai wakuu walileta fujo. *Taifa Leo*, 11, 2019.

Wesonga, C. (2018). Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini. *Taifa Leo*, 14, 2018

# KIAMBATISHO A

## PICHA ZA MAGAZETI YA VICHWA VYA HABARI ZA SIASA TEULE VYENYE UHUSIKA LENGWA

### 1. Uhusika Kiima

a



HABARI ZA KAUNTI

**Musila ajiondoa Wiper baada ya kushindwa katika mchujo**

Na CHARLES WASONGA

NAIROBI

28/4/2017

b



TAIFA LEO Jumanne, Septemba 19, 2017

Wakazi waandamana mahakamani kumtaka akome kupinga ushindi wa gavana

**Karua asukumwa kuondoa kesi yake dhidi ya Waiguru**

19/9/2017

c



**Mawaziri 13 watemwa na Uhuru**

6/1/2018


d

SITANGATANGI, RUTO AJITETEA

3/6/2018


e

Raila akemea Matiang'i

10/01/2019

2. **Uhusika Mahali**


a

Uhuru na Ruto warudi Pwani kutafuta kura

14/3/2017

b


...unga Uhuru wakisema Kalonzo Musyoka amekuwa mzigo...

# Viongozi wa Ukambani wakutana na Rais ikulu

LUCY KILALO na MOHAMED AHMED

12/9/2017

c


...LEO Jumamosi, Aprili 14, 2018

...aila, mkewe Ida wanahudhuria maziko ya Winnie Mandela

# Raila aenda kuwakilisha nchi mazishini

Na CHARLES WASONGA

NAIROBI

14/4/2018

d


# Madiwani kustarehe Dubai bajeti ikikashifiwa

Na ALEX NJERU

WAWAKILISHI watano na spika wa Bunge la Kaunti ya Tharaka-Nithi Jumapili usiku waliondoka nchini kuelekea Dubai huku utata ukizidi kuzingira bajeti iliyosomwa ya mwaka 2018/19 inayodaiwa kuyabagua baadhi ya ...

... wa mbele katika kupitisha bajeti iliyotua mgawanyiko na malalamishi kutoka kwa umma," akasema Charles Nyaga diwani wa Mitheru.

Aidha, alidai kuwa ... kila diwani anayeshiri... wa taarifa kutoka kwa ...

4/7/2018

e


KURUNZI YA PWANI

# Viongozi wataka Jumwa ang'olewe uongozini

Na CHARLES LWANGA

KILIFI

28/10/2019

## 3. Uhusika Yambwa

a




16/1/2017

b




3/12/2017

c




5/1/2018



d

Viongozi wasema eneo la Mlima Kenya litamuunga

# Ruto atetewa kuhusu 2022

HAKI: Kesi ya uchaguzi wa ubunge kuamuliwa baa

9/1/2018



e

# Chama cha Jubilee chateua mwanawe Too kuwa diwani

Na DENNIS LUBANGA UASIN GISHU

4/9/2019

## 4. Uhusika Tendea



a

# Wezi waburudika kabla kuibia mwanasiasa

Na ERIC WAINAINA

3/12/2017



b

dadisi wasema hatua hiyo ni ishara kwamba viongozi wamekosa kuafikiana ikiwa wataunga mkono Uhuru au Raila

# Uamuzi wa Kanu kutoteua mwaniaji wakanganya na kuzua mgawanyiko

12/2/2019

c



Uhuruto wamefanya nifilisike, afichua Joho

Na MWANDISHI WETU

MOMBASA

hangaishwa chini ya uongozi wake.

22/7/2017

d



Jumatatu, Januari 15, 2018 TAIFA LEO

Tunawaonyesha watoto wetu mfano mbaya maishani kwa utundu huu

Si ustaarabu wanasiasa kutimua walimu wanya

22/7/2017

d



Rais atuza kijana gari atafutie riziki

Wafanyabiashara kortini kupinga marufuku

MUULIZE MJUAJI KOMBO

1/6/2018

e



Uhuru aliteua Nyachae kama njia ya kumzawadi

Na WANDERI KAMAU

25/2/2018

## 5. Uhusika Tokeo



a

...sema nia ni kuzuia mshindi katika raundi ya kwanza kwenye uchaguzi ujao

# Wapwani wabuni muungano wao

20/ 2/2017



b

# Mudavadi kuongoza kampeni za NASA

Na VALENTINE OBARA

Mshangao huku watoto watatu wa mwaniaji udiwani waliotoweka wakipatikana mtoni wameuawa

Kenneth atoa ahadi kubwa kwa wakazi akiwa gavana

20/5/2017



c

# Miguna ageuzwa kipenzi cha Raila

Sababu ya kumtimua Miguna

8/2/2018



d

# Misururu ya kashfa haimbanduki Keter

Na WANDERI KAMAU

ALIPOKAMATWA mnamo Ijumaa kwa kuwasilisha stakabadhi zinazodaiwa kuwa ghushi katika Benki Kuu ya Kenya, mbunge Alfred Keter wa Nandi Hills aliongeza msururu wa sakata ambazo zimekuwa zikimwandama.

...amalie mpangilio wa uongozi wa bunge, kwani hii ni taasisi huru," akasema Bw Keter.

Licha ya hayo, aliondolewa katika nafasi hiyo, baada ya wabunge wa kupiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Wabunge wengine waliokaidi agizo hilo ni mbunge...

19/2/2018

e



ila, Matiang'i na Kibicho wadaiwa kuhusika kwenye ghasia zilizokumba

Tangatanga yadai wakuu walileta fujo

13/11/2019

## 6. Uhusika Ala

a



A LEO Jumamosi, Oktoba 21, 2017

Uchunguzi wabaini Okoth, 18, alipigwa risasi mara kadhaa

Mwanafunzi aliuawa kwa risasi- Ripoti

21/10/2017

b



CA ilidai ishara zilionyesha hakuna aliyeponea kifo

5 wahofiwa kufa ajali ya helikopta

Na WAANDISHI WETU

22/10/2017

c


Jumatano, Januari 24, 2018 TAIFA LEO

NASA waache mizaha ya kutumia Biblia kujiapisha

24/1/2018

d


zasema alenga kufurusha maafisa wasio waaminifu kwa utawala wa

Shoka la Obado latia hofu maafisa wakuu

1/11/2018


e


Teknolojia ya Blockchain itumiwe kuzima ufisadi

17/7/2019

# KIAMBATISHO B

# KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA CHUONI



KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 30th November, 2020

TO: Fidelis Kioko Mutuku
C/o Kiswahili Department.
Kenyatta University.

REF: C50/39142/2017

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH MASTERS PROPOSAL

We acknowledge receipt of your revised Proposal as per our recommendations raised by the Graduate School Board at its meeting of 11th September, 2020, Entitled, **"Uhusika Katika Vichwa Vya Habari Vya Siasa Kwenye Gazeti la Taifa Leo (2017-2019)".**

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking Forms per semester. The form has been developed to replace the Progress Report Forms. The Supervision Tracking Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

02 DEC 2020

HARRIET ISABOKE
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

C.c. Chairman, Department of Kiswahili

Supervisors:

1. Dr. Jacktone Onyango
   C/o Department of Kiswahili
   Kenyatta University

2. Dr. Leonard Chacha Mwita
   C/o Department of Sociology, Gender & Dev. Studies
   Kenyatta University

HI/nn

## KIAMBATISHO C

## KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **401386**

Date of Issue: **23/September/2021**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. Fidelis kioko Mutuku of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: UHUSIKA KATIKA VICHWA VYA HABARI VYA SIASA KWENYE GAZETI LA TAIFA LEO (2017-2019) for the period ending : 23/September/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/13026**

**401386**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.